# Nipashe

Jumamosi Mei 6, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581302

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


SUPA JACKPOT

TZS. 1,109,975,029

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#





## Mwalimu matatani madai kuhatarisha maisha wanafunzi

UKURASA 3

# Sababu mzee na wanawe watatu kujiua kwa moto

UKURASA 2





Waombolezaji wakiwa nyumbani kwa marehemu Amani Madumba katika kijiji cha Malolo, Kilosa mkoani Morogoro jana, aliyejifungia chumbani na watoto wake watatu kujiteketeza kwa moto. **Picha ndogo**, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro, ACP Alex Mkama, akiwa eneo la tukio na mabaki ya miili ikiwa imefunikwa kitandani. **PICHA: IDDA MUSHI**

UKURASA 3

## TUCTA yasifu usiri nyongeza mishahara ya wafanyakazi



## ACT yataka FCC ijiuzulu sakata la Tanga Cement, serikali yajibu

UK. 2 & 7


**MICHEZO** **YANGA: MARUMO HAWACHOMOKI** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Kivuli wa Wizara ya Madini wa Chama cha ACT-Wazalendo, Edga Mkosamali (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana wakati wa uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, iliyowasilishwa bungeni hivi karibuni. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# ACT yaikaba koo FCC sakata la uuzwaji wa Tanga Cement

**Na Mwandishi Wetu**

SAKATA la uuzwaji wa Kampuni ya Saruji ya Tanga limezidi kuota mizizi baada ya Chama cha ACT - Wazalendo kuibuka na kuitaka Tume ya Ushindani (FCC) kujiuzulu kwa kile ilichosema ni kufanya kosa la kukaidi amri ya Baraza la Ushindani wa Biashara (FCT).

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara, Halima Nabalang'anya, kuhusu mpango wa Wizara ya Uwekezaji,Viwanda na Biashara kwa mwaka 2023/24, alisema pamoja na mambo mengine serikali inapaswa kuhakikisha inalinda viwanda vya mji wa Tanga kwa kushawishi kampuni kuanzisha viwanda vingine ili kuongeza washindani katika soko la saruji nchini.

Akizungumza kuhusu mgogoro wa utwaaji wa Tanga Cement, alisema kumekuwapo na mivutano, mijadala na mabishano miongoni mwa wadau kuhusu uamuzi wa FCC kuidhinisha muungano wa Twiga Cement na Tanga Cement.

Nabalang'anya katika taarifa iliyotolewa kwa niaba yake na Waziri Kivuli wa Madini wa chama hicho, Edgar Mkosamali, alisema uamuzi huo ulitokana na makubaliano yaliyofanyika mapema Oktoba 2021, kati ya Scancem International DA (Scancem) - kampuni tanzu ya Heidelberg Cement AG, inayomiliki Twiga Cement na AfriSam Mauritius Investment Holdings Limited, inayomiliki Tanga Cement kwa kukubali kuuza asilimia 68.33. hisa za Tanga Cement.

Alisema msingi wa mgogoro ulitokana na uamuzi huo FCC kukubali Muungano ulifanywa kinyume cha sheria na taratibu za soko la ushindani nchini.

Kwa mujibu wa Nabalang'anya, Sheria ya FCC inahitaji ubia wowote usizidi kiwango cha juu cha asilimia 35 ya hisa ya soko ili kuhakikisha ushindani wa haki unakuwapo.

"Kutokana na uamuzi huo wa awali wa FCC, wadau walijitokeza kuupinga kwa kukata rufani FCT chombo ambacho kina hadhi ya kimahakama katika masuala ya ushindani. Hatimaye, Septemba 23, 2022 uamuzi wa kuruhusu muungano huo ulibatilishwa na chombo hicho," alisema.

Alisema mgogoro mpya uliozaliwa na unaoendelea sasa, ulitokana na FCC kufanya ukiukwaji wa sheria na kuonyesha dharau za wazi kwa FCT.

"Kwa kuanzishwa upya kwa zabuni ya uuzaji wa hisa za Twiga Cement mwishoni mwa Desemba, 2022 na Februari 11, 2023 FCC iliweka tangazo kwa umma kupata maoni ya wadau juu ya kuendelea na uamuzi wa kuuza hisa hizo. Kuendelea kwa mchakato huo licha ya uamuzi wa mahakama ni kiashiria kuwa kuna mgongano wa kimaslahi ulioonyeshwa na FCC hata kukubali kuvunja sheria za nchi," alisema.

Nabalang'anya alisema sekta ndogo ya viwanda vya saruji ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya nchi, hivyo unatakiwa uangalifu mkubwa katika kuchukua uamuzi wowote kwenye tasnia hiyo.

"Uzalishaji na soko lake linapaswa kuendeshwa kwa mujibu wa taratibu na sheria ili kuhakikisha hakutokei majanga ya uhaba, uhodhi wa soko na hatima ya upatikanaji wa saruji kuwekwa kwenye mikono ya mtu mmoja. Uamuzi wa FCC kuidhinisha utwaaji wa Tanga Cement kwa Twiga Cement si tu unakiuka sheria bali unaonyesha wazi athari za kuacha hatima ya soko la saruji kwenye uamuzi wa kampuni moja jambo ambalo si afya kwa maendeleo ya watu," alisisitiza.

Alisema Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara katika mpango wake wa bajeti 2023/24 licha kelele zilizopigwa na wabunge, wananchi na wadau wengine, haijatoa uamuzi wowote katika kuhakikisha mazingira ya uwekezaji na uratibu wa biashara ya ushindani yanakuwapo.

"Wizara ndiyo inaratibu na kuisimamia FCC. Kukaa kimya ni kama inabariki kuvunjwa kwa taratibu na sheria za nchi. Hii ni kuandaa mazingira ya kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi siku za usoni,"alisema.

"ACT - Walendo tunaishauri serikali isimamishe mchakato kwa lengo la kuanzisha upya kwa uwazi na kwa kuzingatia sheria za nchi yetu," alisema.

**MWIJAGE AHADHARISHA**

Akichangia juzi mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, viwanda na Biashara kwa mwaka 2023/24, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage, alitoa tahadhari kuhusu mchakato huo.

Mwijage ambaye aliwahi kuwa Waziri wa viwanda na Biashara katika serikali ya awamu ya tano, alisema tahadhari isipochukuliwa, kuna uwezekano wa kukosekana kwa saruji au kupanda kwa bei kutokana na ukiritimba katika soko.

Alisema kunapokuwa na muunganoko wa kampuni na wahusika katika soko wakawa wachache kuna uwezekano wa kuwaumiza watumiaji wa bidhaa. Pia alisema kuna hatari ya kukosekana kwa bidhaa na matokeo yake nchi kuagiza bidhaa kutoka nje tena kwa kutumia fedha za kigeni.

Kauli hiyo ya Mwijage iliungwa mkono na Mbunge wa Mlimba (CCM), Godwin Kunambi, aliyesema kununua kwa wingi bidhaa kutoka nje kunaweza kusababisha mfumuko wa bei na kuyumba kwa mitaji (capital flow inflation).

# Sababu mzee na watoto kujiua kwa moto yatajwa

**Na Idda Mushi,** MIKUMI

MZEE wa miaka 72, Amani Madumba, na watoto wake watatu, wamefariki dunia kwa madai ya baba huyo kuchoma moto nyumba waliyokuwa wakiishi katika kijiji cha Malolo B, Tarafa ya Mikumi, Kilosa mkoani Morogoro kwa kile kilichodaiwa ugumu wa maisha.

Watoto waliofariki dunia katika tukio hilo ni, Bahati Amani (5), Sadick Amani (8) na Habibu Amani (10).

Kwa mujibu wa mjukuu wa Madumba, Edina Madumba, ambaye alikuwa akiishi kwenye chumba cha jirani, aliiambia Nipashe jana kuwa babu yake alikuwa anakabiliwa na ugumu wa maisha.

"Babu alikuwa anaishi maisha magumu na alikuwa akisaidiwa TASAF (Mfuko wa Maendeleo ya Jamii). Alikuwa na tatizo la kiafya, alikuwa na tatizo la figo na alianza kuchangisha fedha ili aende kutibiwa. Ninafiri babu ameamua kuchukua uamuzi huu kutokana na ugumu wa maisha.

"Tangu mke wake wa kwanza afariki dunia, maisha ya babu yaliyumba. Labda ameona kutokana na maisha yake kuwa magumu, ameamua kuchukua uamuzi huu maana watoto wake walikuwa wakienda kwa mama yao. Mama alikuwa anawafukuza warudi kwa baba yao kutokana na ugumu wa maisha," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi (ACP) Alex Mkama, na timu yake walifika eneo la tukio kwa ajili ya taratibu za kisheria na alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana.

Alisema chanzo cha awali cha tukio hilo kinasadikika kuwa ni ugumu wa maisha ingawa uchunguzi zaidi unaendelea.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Malolo B, Sufiani Ndagama, alisema alipata taarifa za tukio hilo usiku wa kuamkia jana majira ya saa 7:04 baada ya kufuatwa nyumbani kwake na baadhi ya wanafamilia wa marehemu.

Ndagama alisema baada ya kufika eneo la tukio alikuta wananchi wakiendelea kuuzima moto huo na walipofanikiwa na kuingia ndani walikuta miili ya watu wanne.

"Huyu baba alikuwa anaishi na watoto wake tu. Alizaa na mwanamke lakini kila mmoja alikuwa anaishi kwake. Watoto walikuwa wakishinda kwa mama yao mchana na ilikuwa ikifika jioni wanarudi kulala kwa baba yao," alisema Ndagama.

Alisema mwanamume huyo alikuwa na mke wa kwanza ambaye alizaa naye watoto ambao kwa sasa ni wakubwa na alipofariki dunia, ndipo alipozaa na mwanamke mwingine watoto hao waliofariki dunia kwenye tukio hilo.

"Wawili hawa tangu waanze uhusiano na kuzaa watoto hawa, sijawahi kusikia ugomvi mkubwa baina yao. Labda ugomvi wa kawaida wa mke kuhitaji mahitaji kama chakula na mzee kushindwa kutoa kutokana na hali ya kiuchumi. Siamini kama ndiyo sababu ya kuchukua uamuzi huu mgumu," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema walifanikiwa kuuzima moto huo kwa kushirikiana na askari kutoka mkoa wa Iringa ambao wanapakana nao eneo la tukio, baada ya kusubiri askari kutoka Mikumi ambao waliwaarifu kuwa walikuwa njiani pamoja na madaktari.

Kiongozi huyo alisema nyumba waliyokuwa wakiishi imejengwa kwa udongo na kuezekwa kwa mabati na walikuta miili yote imeungua vibaya na wakati huo wanasubiri taratibu za kisheria zifanyike ili kuizika.

Baadhi ya majirani, Sebastian Sebastian na Elinazi John, walisimulia kwamba walisikia kelele za kuomba msaada na walipofika eneo la tukio walikuta tayari moto ni mkubwa na mlango wa nyumba ulikuwa umefungwa kwa ndani.



Sehemu ya familia 47 zikiwa nje chini ya miti katika mtaa wa Sulungai, kata ya Ipagala, jijini Dodoma jana, baada ya nyumba nane kubomolewa na dalali wa Mahakama kwa madai kuwa zimejengwa kwenye eneo la taasisi ya kidini, kwa zaidi ya wiki moja sasa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TUCTA yasifu usiri nyongeza za mishahara ya wafanyakazi

**Na Beatrice Shayo**

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), limesema limefurahishwa na kitendo cha Rais Samia Suluhu Hassan cha kutotaja nyongeza za mshahara hadharani, jambo ambalo imesema limetoa fursa ya kukaa meza moja kujadili kilichopangwa.

Kaimu Katibu Mkuu wa TUCTA, Said Wamba, alisema jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari huku akisema watakutana na wahusika wanaopanga nyongeza hiyo, ili kujua kinachopangwa na kujadiliana.

"Tumemshukuru Rais Samia kuficha. Angetamka nyongeza ya mshahara ingekuwa vigumu kupata nafasi ya kujadili, alichokifanya ametupa fursa.

"Kwa sasa sisi ni kukimbilia katika ofisi hizo mapema. Kama angesema mfano mtapata asilimia 20, mtajadili akishasema? Sasa tunayo nafasi ya kujadiliana, kuna watu wanasema Rais hakutamka labda kuna kitu anahofia. Sisi tunaamini ametoa nafasi nzuri kwetu kugonga hodi na kuzungumza kwa pamoja na kufikia muafaka," alisema.

Wamba alisema mwaka jana alitangaza na kilichotokea ni malalamiko kutokana na nyongeza hiyo iliyotangazwa, hivyo kuibadili inakuwa ni vigumu.

Alisema kazi kubwa waliyokuwa nayo kama vyama vya wafanyakazi ni kugonga hodi katika ofisi za serikali zinazotayarisha mishahara na mambo mengine ili wafanye kazi hiyo kwa pamoja.

"Tusingoje kitu kimetangazwa ndio tuanze kulalamika. Hapo tunakuwa tumechelewa na hakuna mabadiliko ambayo serikali inaweza kuyafanya, ni vizuri vikao vya ndani vinavyoandaa mishahara na mambo mengine na sisi tushiriki tuone mambo yanavyokwenda yanaendana na yale ya hutuba ya Rais," alisema.

Alisema wanaiandikia barua Ofisi ya Waziri Mkuu na wizara zingine ambazo zinahusika, kuwaarifu ajenda na mambo mbalimbali ambayo Rais aliyatolea maelekezo.

"Watuambie tunakaa lini ili mambo yanavyotoka yakiwa na makubaliano ya vyama vya wafanyakazi na serikali hii ndio kazi kubwa tuliyokuwa nayo kwa sasa.

"Bado tuna tatizo kubwa kwa wafanyakazi kujali muda. Muda ni jambo muhimu ni kigezo muhimu katika kupima ufanisi, tija na maendeleo ya nchi. Unatumiaje muda? Kitu ambacho ni hadimu ndani ya dunia,"alisema.

Wamba alisema endapo wafanyakazi wangekuwa wanapimwa kwa muda ni wachache wangepata mshahara kamili ambao anaufanyia kazi.

Pia alisema kuna shida katika maadili ya utendaji kazi wa wanachama wao na hilo hawawezi kulikwepa na wana wajibu wa kudai nyongeza ya mshahara. Alisema kuna haja ya serikali kufanya maboresho ya viwango vya kodi kwa wafanyakazi wa umma sambamba na mikataba ili kuboresha hali bora kwa wafanyakazi wa umma.

Alisema wafanyakazi ni walipa kodi wakubwa hivyo serikali iwatazame na kuacha kuwaandama na kodi nyingi ambazo zinakwenda kupunguza mishahara yao.

"Tunaiomba serikali ijaribu kutizama upya sheria na mifumo ya kodi ili iweze kutoa nafuu fulani kwa wafanyakazi. Haya ni miongoni mwa mambo tukayokwenda kuyafuatilia kuanzia sasa ikiwamo la bima ya afya, sheria za kazi bila kusubiria sherehe za Mei Mosi," alisema.

Katika hatua nyingine, TUCTA imesema inafuatilia sakata la zaidi ya wanachama 70 wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) Mkoa wa Mbeya ambao walitelekezwa na viongozi wao katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine siku ya Mei Mosi, bila kulipwa posho wala kupatiwa chakula.

Wamba alisema kwa sasa wanamtafuta Katibu Mkuu wa TALGWU kwa ajili ya mazungumzo ya jambo hilo ili kurekebisha makosa yaliyojitokeza.

# Mwalimu matatani kwa madai kuhatarisha maisha wanafunzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia mwalimu wa Shule ya Msingi Generation ya jijini hapa, Baraka Nkoko, kwa tuhuma za kuhatarisha maisha ya wanafunzi kwa kuwarundika kwenye gari dogo, hali iliyosababisha baadhi yao kuzirai kwa kukosa hewa.

Mwalimu huyo anadaiwa kuwarundika wanafunzi 27 kwenye gari ndogo aina ya Toyota NADIA na kuwasafirisha huku akiwa amefunga vioo, hali ambayo iliwafanya wanafunzi hao kushindwa kupumua vizuri.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama barabarani wa Mkoa wa Mbeya, Mrakibu wa Polisi (SP) Yusuf Kamotta, aliyasema hayo juzi wakati maofisa wa jeshi hilo walipokuwa wanatoa mafunzo maalumu ya usalama wa watoto kwa wakuu wa shule, walimu wakuu pamoja na wamiliki wa shule.

Kamotta alisema watoto hao baada ya kukosa hewa, walianza kulia ndipo mwalimu huyo akaamua kuegesha gari pembezoni mwa barabara kwa lengo la kuangalia hali zao.

Alisema wakati mwalimu huyo anawangalia watoto hao kuna msamaria mwema aliona kitendo hicho akatoa taarifa polisi ndipo wakaanza kumfuatilia mpaka wakamkuta na kumtia mbaroni.

"Tukio hili lilitokea jumatatu wakati tupo kwenye kikao, msamaria mwema alipoona kitendo hicho alitoa taarifa kwa Afande RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa, Benjamin Kuzaga) ambaye alinituma nikafuatilie. Tulikwenda tukamkuta na tulibaini kuwa baadhi ya watoto walikuwa wamepelekwa zahanati," alisema Kamotta.

Kutokana na tukio hilo, alisema waliamua kwenda kufuatilia kwenye zahanati walikokuwa wamepelekwa watoto hao na kuwakuta sita kati yao ambao walikuwa wamezidiwa wakipatiwa huduma ya kwanza na wahudumu wa zahanati hiyo.

Aidha, Kamotta aliongeza kuwa walimkamata mwalimu huyo na kumpeleka mahabusu na wanakusudia kumfikisha mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine.

Pia alisema alisema maofisa wa jeshi hilo waliamua kukagua magari ya shule hiyo wakabaini kuwa ni machache na ni madogo kiasi kwamba hayaendani na idadi ya wanafunzi waliopo.

Akizungumza na walimu pamoja na wamiliki wa shule, Kamotta aliagiza magari yote ya shule kupakwa rangi ya njano ili iwe rahisi kutambuliwa na wadau na kurahisisha ufuatiliaji wa mwenendo wa wahudumu wa magari hayo.

Pia aliwataka wamiliki wa shule kuajiri wahudumu wa kike kwenye magari ya wanafunzi ambao watakuwa wanahakikisha watoto wote wanaopanda kweye magari hayo wanafika salama nyumbani kwao kwa maelezo kuwa wao wana uchungu zaidi na watoto kuliko wanaume.

"Kuna dereva mmoja wa gari la shule alikuwa anawapeleka wanafunzi wote halafu anambakiza mmoja wa kiume kisha anamfanyia vitendo vya ukatili. Sasa ili tuandae kizazi kizuri cha baadaye, ni vyema tuwatumie wahudumu wa kike," alisema Kamotta.

Alisema jeshi hilo litaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuwalinda watoto na kwamba wataendelea kufanya ukaguzi wa magari ya shule ili kuepusha maafa kama yaliyowahi kutokea Mtwara na Arusha.

**TANGAZO**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF WORKS & TRANSPORT**
**TANZANIA NATIONAL ROADS AGENCY**
**REGIONAL MANAGER'S OFFICE - TANROADS COAST**

**Ref. No: AB.267/322/01/168** **Date: 06TH May, 2023**

Tanzania National Roads Agency — TANROADS — Good roads for national development

# RE – ADVERTISE - JOB VACANCIES ANNOUNCEMENT

Tanzania National Roads Agency (TANROADS) is an Agency under the Ministry of Works and Transport which is responsible for the Development and Maintenance of the Trunk and Regional Roads Network in Tanzania Mainland. Apart from this is also responsible in conducting Axle Load Control Operations and Airport Construction.
Tanzania National Roads Agency (TANROADS) on behalf of the Government of the United Republic of Tanzania entered into a Contract for the **UPGRADING OF NYAMWAGE – UTETE ROAD (33.7 KM) TO BITUMEN STANDARD CONTRACT NO: TRD/HQ/1036/2022/23**

As a measure to strengthen Capacity of discharging TANROADS' functions effectively, the Regional Manager's Office TANROADS – Coast, on behalf of Chief Executive, seeks to recruit qualified and competent Tanzanian Citizen to fill Vacancy posts for the specific duties on short term basis.
Applications are invited from suitably qualified and competent Tanzanian to fill vacancies in the Region. Successful applicants must be ready to work for considerable length of time in Coast Region within the project area when situations warrant.

**TERMS AND CONDITIONS OF SERVICE**
Appointment will be on Contract Terms of One (1) year renewable subject to satisfactory performance, efficiency and effectiveness.

**1. HIGHWAY ENGINEER (1 Post)**
The Highway Engineer shall be fully responsible for the supervision of the construction in accordance with the provision of Contract. He/She shall supervise the construction works with due diligence and efficiency and in accordance with sound technical, administrative, financial and economic practices. He/She shall perform all duties associated with such tasks to ensure that only the best construction practices are followed and that the final product is in all respects equal to, or better than that specified, at the most economic costs and is carried out in full compliance with the governing specifications.
She/he must be a registered Professional Civil Engineer with a degree in Civil Engineering or Highway Engineering. Postgraduate qualification in Highway Engineering is an added advantage. She/he must have a minimum of Ten (10) years of specific experience related to road design and construction supervision. She/he must have served in a similar capacity on at least two (2) projects for construction of bituminous roads of similar magnitude and complexity in the last 10 years. His/Her duties shall comprise road surveys, construction of pavement structure, measuring of quantities and management of site operations. In addition, he/she must have a working experience of at least 3 years in Sub-Sahara countries. Proficiency in written and spoken English is mandatory.

**2. MATERIALS ENGINEER (1 Post)**
The Soils/Materials Engineer shall be responsible for conducting and supervising the materials investigation with a view to achieving optimal design and construction strategy. The Soil/Materials Engineer shall carry out the pavement design and should be conversant with current practice in testing and pavement construction techniques.
She/He must be a registered Professional Civil Engineer with a degree in Civil Engineering or Pavement or Materials Engineering. Postgraduate qualification in Pavement or Materials Engineering is an added advantage. She/He must have a minimum of Ten (10) years of specific experience in Pavement/Materials matters related to road works. She/He must have served in a similar capacity on at least two (2) road projects of similar magnitude and complexity in the Last 10 years. She/He shall be responsible for ensuring the quality of all materials to be incorporated in the works, as well as the completed works, conform to the contract specifications. In addition, He/She must have a working experience of at least 3 years in Sub-Sahara countries. Proficiency in written and spoken English is mandatory.

**3. BRIDGE/DRAINAGE ENGINEER (1 Post)**
The Bridge/Drainage Engineer shall be fully responsible for structural analysis, designing of bridge/drainage elements and detailing. He/She will be responsible for the assessment of existing Bridges and design of new Bridges and all drainage structures along the project road including submission of the report. He/She should have the ability to read and interpret project specifications.

He/She must possess Degree in Civil Engineering or an equivalent qualification. He/She must have at least Ten (10) of specific experience in road design related to similar assignment. He/She must have served as a Bridge/Drainage Engineer on at least two (2) projects of similar magnitude and complexity within the last 10 years. Post graduate qualification in Structural/Bridge Engineering is an added advantage. Knowledge in computer applications and fluency in written and spoken English are mandatory.

**4. TOPOGRAPHICAL SURVEYOR (1 Post)**
The Topographical Surveyor shall be fully responsible for conduction and supervising the survey team. He/She will be responsible for planning of the fieldwork, select known survey reference points, and determine the precise location of important features in the survey area. He/She shall be responsible for searching legal records, look for evidence of previous references survey points (geodetic reference points and national benchmarks) and analyses the data to determine the location of boundary lines and record the results of the results of the survey, verify the accuracy of data, and prepare plans, maps and reports.
He/She must possess a minimum of Diploma in Land Surveying. She/He must be a registered Land Surveyor. She/He must have Eight (8) years specific experience in road design and construction. She/He must have served in a similar capacity on at least two (2) road construction projects of similar magnitude and complexity within the last 10 years. In addition, He/She must have a working experience of at least 3 years in Sub-Sahara countries. Proficiency in written and spoken English is mandatory.

**5. ASISTANT SURVEYOR (1 Post)**
The Assistant Surveyor shall be fully responsible for conduction and supervising the survey team. He/She will be responsible for planning of the fieldwork, select known survey reference points, and determine the precise location of important features in the survey area. He/She shall be responsible for searching legal records, look for evidence of previous references survey points (geodetic reference points and national benchmarks) and analyses the data to determine the location of boundary lines and record the results of the results of the survey, verify the accuracy of data, and prepare plans, maps and reports.

She/He must have a holder of Diploma (NTA Level 6) in Land Surveying. She/He must have Five (5) years specific experience in road design and construction. She/He must have served in a similar capacity on at least two (2) road construction projects of similar magnitude and complexity within the last 2 years. In addition, He/She must have a working experience of at least 3 years in Sub - Sahara countries. Proficiency in written and spoken English is mandatory.

**6. CAD TECHNICIAN (1 Post)**
The CAD Expert shall be fully responsible for roads and bridges CAD Drawings, preparing and running Animations for the projects.
She/He must possess a minimum of Diploma in Civil or Highway Engineering from recognized Institution. She/He must be a registered with ERB as Civil Technician. She/He must have five (5) years specific experience in drawing and drafting of Road/Highway Works and construction. She/He must have served in a similar capacity on at least two (2) road construction projects in the Last 5 years. In addition, He/She must have a working experience of at least 3 years in Sub-Sahara countries. Proficiency in written and spoken English is mandatory.

**GENERAL CONDITIONS**
i. Applicants must attach an up – to date Curriculum Vitae (CV) having reliable contacts: postal address/post code, e – mail and telephone numbers
ii. Applicants should apply on the strength of the information given in this advertisement;
iii. Applicants must attach their certified copies of the following certificates:
a. Degree/Advanced Diploma/Diploma;
b. Form IV and Form VI National Examination Certificates;
c. Professional Registration and Training Certificates from respective Registration Regulatory Bodies, (where applicable);
d. Birth Certificate;
iv. Submission of the following documents is strictly not acceptable;
a. Form IV and Form VI results slips;
b. Testimonials and all partial transcripts
v. An applicant should indicate three relevant referees with their reliable contacts;
vi. Certificates from foreign examination bodies for Ordinary, Advanced level or universities/colleges should be authenticated by the National respective organs (NECTA, NACTE or TCU)
vii. A signed APPLICATION LETTER should be in English
viii. ANY ELECTRONIC SUBMISSION SHALL NOT BE CONSIDERED
ix. Deadline for the submission of application is 19th May, 2023
x. Only short-listed candidates will be informed for interview and;
xi. Presentation of forged certificates and other information will render to necessitate legal action;

**ALL APPLICATIONS MUST BE POSTED TO THE ADDRESS BELOW:**

**Regional Manager,**
**TANROADS,**
**P. O BOX 30150,**
**COAST.**

***NOTE: Hand delivery shall NOT be accepted***

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF WORKS & TRANSPORT**
**TANZANIA NATIONAL ROADS AGENCY**
**REGIONAL MANAGER'S OFFICE - TANROADS COAST**

**Ref. No: AB.267/322/01/169** **Date: 06Th May, 2023**

# RE – ADVERTISE JOB VACANCIES ANNOUNCEMENT

Tanzania National Roads Agency *(TANROADS)* is an Agency under the Ministry of Works and Transport which is responsible for the Development and Maintenance of the Trunk and Regional Roads Network in Tanzania Mainland. Apart from this is also responsible in conducting Axle Load Control Operations and Airport Construction.

Tanzania National Roads Agency *(TANROADS)* on behalf of the Government of the United Republic of Tanzania entered into a Contract for the **FOR CONSTRUCTION OF MBAMBE BRIDGE (81M) AND ITS APPROACH ROADS (3.0 KM) TO BITUMEN STANDARD CONTRACT NO: TRD/HQ/1037/2022/23/CR/W/64**

As a measure to strengthen Capacity of discharging TANROADS' functions effectively, the Regional Manager's Office TANROADS – Coast, on behalf of Chief Executive, seeks to recruit qualified and competent Tanzanian Citizen to fill Vacancy posts for the specific duties on short term basis.

Applications are invited from suitably qualified and competent Tanzanian to fill vacancies in the Region. Successful applicants must be ready to work for considerable length of time in Coast Region within the project area when situations warrant.

**TERMS AND CONDITIONS OF SERVICE**
Appointment will be on Contract Terms of One (1) year renewable subject to satisfactory performance, efficiency and effectiveness.

1. **HIGHWAY ENGINEER (1 Post)**
   The Highway Engineer shall be fully responsible for the supervision of the construction in accordance with the provision of Contract. He/She shall supervise the construction works with due diligence and efficiency and in accordance with sound technical, administrative, financial and economic practices. He/She shall perform all duties associated with such tasks to ensure that only the best construction practices are followed and that the final product is in all respects equal to, or better than that specified, at the most economic costs and is carried out in full compliance with the governing specifications.
   She/He must be a registered Professional Civil Engineer with a degree in Civil Engineering or Highway Engineering. Postgraduate qualification in Highway Engineering is an added advantage. She/He must have a minimum of Seven (7) years of experience related to road design and construction. He/She must have served in a similar capacity on at least two (2) projects for construction of Bituminous roads of similar magnitude and complexity in the last 7 years. She/He duties shall comprise road surveys, construction of pavement structures, measuring of quantities and management of site operations. In addition, He/She must have a working experience of at least 3 years in Sub-Sahara countries. Proficiency in written and spoken English is mandatory.

2. ***MATERIALS ENGINEER (1 Post)***
   The Soils/Materials Engineer shall be responsible for conducting and supervising the materials investigation with a view to achieving optimal design and construction strategy. The Soil/Materials Engineer shall carry out the pavement & Bridge design should be conversant with current practice in testing and pavement construction techniques.
   She/He must be a registered Professional Civil Engineer with a degree in Civil Engineering or Pavement or Materials Engineering. Postgraduate qualification in Pavement or Materials Engineering is an added advantage. She/He must have a minimum of Seven (7) years of experience in Pavement/Materials matters related to road works. She/He must have served in at least two (2) road projects of similar magnitude and complexity in the Last 7 years. She/He shall be responsible for ensuring the quality of all materials to be incorporated in the works, as well as the completed works, conform to the contract specifications. In addition, He/She must have a working experience of at least 3 years in Sub-Sahara countries. Proficiency in written and spoken English is mandatory.

3. **BRIDGE/DRAINAGE ENGINEER (1 Post)**
   The Bridge/Drainage Engineer shall be fully responsible for structural analysis, designing/design review of bridge/drainage elements detailing and supervision of works. He/She will be responsible for the assessment of existing Bridges, design of new Bridges and all drainage structures along the project road including submission of the report. He/She should have the ability to read and interpret project specifications.

   He/She must be a registered Civil Engineer with a Degree in Civil Engineering or Bridge Engineering or Structural Engineering. He/She must have a minimum of Seven (7) of experience in bridge and construction. He/She must have experience of Bridge and road works of similar nature (Piled foundation Bridges). He/She shall be responsible for ensuring the bridges and other drainage structures are constructed according to design and conform to the contract specifications. In addition, He/She must have working experience of at least 3 years in Sub-Saharan Countries. Proficiency in written and spoken English are mandatory.

4. **TOPOGRAPHICAL SURVEYOR (1 Post)**
   The Topographical Surveyor shall be fully responsible for conduction and supervising the survey team. He/She will be responsible for planning of the fieldwork, select known survey reference points and determine the precise location of important features in the survey area. He/She shall be responsible for searching legal records, look for evidence of previous references survey points (geodetic reference points and national benchmarks), analyses the data to determine the location of boundary lines and record the results of the survey, verify the accuracy of data, prepare plans, maps and reports.

   He/She must possess a minimum of Advanced Diploma in Land Surveying. She/He must be a registered Land Surveyor. She/He must have Six (6) years specific experience in road design and construction. She/He must have served in at least two (2) road construction projects of similar magnitude and complexity within the last 6 years. In addition, He/She must have a working experience of at least 3 years in Sub-Sahara countries. Proficiency in written and spoken English is mandatory.

5. **CAD TECHNICIAN (1 Post)**
   The CAD Expert shall be fully responsible for roads and bridges CAD Drawings, preparing and running Animations for the projects.
   She/He must possess a minimum of Diploma in Civil or Highway Engineering from recognized Institution. She/He must be a registered with ERB as Civil Technician. She/He must have five (5) years specific experience in drawing and drafting of Bridge/Road works and construction. She/He must have served in a similar capacity on at least two (2) road construction projects in the Last 5 years. In addition, He/She must have a working experience of at least 3 years in Sub-Sahara countries. Proficiency in written and spoken English is mandatory.

**GENERAL CONDITIONS.**

i. Applicants must attach an up – to date Curriculum Vitae (CV) having reliable contacts: postal address/post code, e – mail and telephone numbers
ii. Applicants should apply on the strength of the information given in this advertisement;
iii. Applicants must attach their certified copies of the following certificates:
a. Degree/Advanced Diploma/Diploma;
b. Form IV and Form VI National Examination Certificates;
c. Professional Registration and Training Certificates from respective Registration Regulatory Bodies, (where applicable);
d. Birth Certificate;
iv. Submission of the following documents is strictly not acceptable;
a. Form IV and Form VI results slips;
b. Testimonials and all partial transcripts
v. An applicant should indicate three relevant referees with their reliable contacts;
vi. Certificates from foreign examination bodies for Ordinary, Advanced level or universities/colleges should be authenticated by the National respective organs (NECTA, NACTE or TCU)
vii. A signed APPLICATION LETTER should be in English
viii. ANY ELECTRONIC SUBMISSION SHALL NOT BE CONSIDERED
ix. Deadline for the submission of application is 19th May, 2023
x. Only short-listed candidates will be informed for interview and;
xi. Presentation of forged certificates and other information will render to necessitate legal action;

**ALL APPLICATIONS MUST BE POSTED TO THE ADDRESS BELOW:**
**Regional Manager,**
**TANROADS,**
**P. O BOX 30150,**
**COAST.**

***NOTE: Hand delivery shall NOT be accepted***

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Yanga malizeni kibarua CAF nchini kuwavuruga Marumo

**WAWAKILISHI** pekee waliobakia nchini katika mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Yanga wamebakiwa na siku tatu za kuianza 'safari' ya kucheza hatua ya fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho kwa kuikaribisha Marumo Gallants kutoka Afrika Kusini.

Yanga imetinga hatua ya nusu fainali baada ya kuwafunga Rivers United ya Nigeria mabao 2-0, lakini pia ndio wawakilishi pekee wa Afrika Mashariki na Kati katika mashindano ya CAF baada ya Simba iliyokuwa ikichuana kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kuondolewa kwenye hatua ya robo fainali wiki iliyopita.

Kuondolewa kwa Simba katika hatua hiyo kubaki funzo kwa Yanga inayopambana kuweka historia ya kufika fainali au kubeba kombe la Afrika kwa kuangalia wapi watani zao waliteleza na ndio iwe ramani yao kufanya vizuri.

Yanga inatakiwa ijipange na kufanyia kazi makosa waliyonayo kabla ya kuwakabili wapinzani wao na hatimaye kufaulu harakati zao za kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Moja ya sababu ambazo zimekuwa zikitajwa Simba kuondolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Wydad Casablanca ni pamoja na ushindi 'finyu' wa bao 1-0 walioupata nyumbani na kujikuta wanaondolewa kwa penalti baada ya wapinzani wao pia kupata bao moja waliporudiana huko Morocco.

Kwa namna Simba walivyocheza kwenye mchezo ule wa marudiano ni wazi kama wangekuwa wamepata ushindi wa angalau mabao 2-0 na kuendelea, sasa hivi wangekuwa wanajiandaa kucheza mechi ya nusu fainali na Waarabu (Wydad Casablanca) wangekuwa wameondolewa katika michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika. Lakini pia ingekuwa imewavua taji mabingwa hao watetezi.

Tumegusia matokeo ya Simba katika safari hii ya Yanga kutinga nusu fainali ili waone umuhimu wa kupata ushindi mkubwa kwenye uwanja wa nyumbani. Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amenukuliwa kwa nyakati tofauti akijipanga kuhakikisha anamaliza kazi kwenye uwanja wa nyumbani (Benjamin Mkapa), kwa kuwa anatambua umuhimu wa matokeo ya ushindi mnono ndani ya ardhi ya nyumbani.

Tunaamini nafasi ya Yanga kufuzu kucheza fainali ya michuano hii namba mbili kwa ukubwa Afrika ni pamoja na kupata ushindi mnono mbele ya mashabiki wao, Yanga jiandaeni kuhakikisha mnawapa furaha mashabiki wenu pamoja na Watanzania kwa sababu sasa hivi mnapeperusha bendera ya nchi na si klabu yenu pekee.

Hakuna kisichowezekana, kikubwa kwa wachezaji na benchi la ufundi ni kujipanga na kujiandaa vyema huku wakijiwekea malengo ya nini wanachokitaka katika michezo hiyo miwili iliyoko mbele yao na hatimaye kukata tiketi ya kucheza fainali.

Hata hivyo, pamoja na ubora wa kikosi cha Yanga kwa sasa na matokeo mazuri waliyoyapata katika michezo iliyopita ya michuano hiyo, bado wanatakiwa kuchukua tahadhari wanapokwenda kuwakabili Marumo Gallants kwani na wao watakuwa wamejiandaa vyema kuwakabili.

Ni ukweli mpaka kufikia hatua hiyo na timu zote nne zilizofuzu kucheza nusu fainali ni timu nzuri na ngumu hivyo hakuna mnyonge, kikubwa ni wachezaji kujiandaa na kuwa tayari kupambania bendera ya timu lakini pia kujitengenezea nafasi za kununuliwa pale watakapowavutia makocha na mawakala wa klabu za nje ya Tanzania na hata Ulaya.

Yanga ifahamu ina nafasi ya kupambana kulipa taifa heshima na kwa kuanza kupata ushindi mnono nyumbani wakiwa ni 'mchezaji wa 12'. Ushindi wa Yanga na kufuzu kwao kucheza fainali sio tu ni sifa kwa timu na mashabiki wao lakini ni sifa kwa taifa kwa kuwa nchi iliyotoa timu kucheza hatua hiyo, lakini pia ni sifa kwa ligi yetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

### Hongera Fountain Gate kujitosa vita ya rushwa

Na Adam Fungamwango

**KWA** muda mrefu katika soka la Tanzania kumekuwa na fununu na tetesi za kuwapo kwa tuhuma za upangaji matokeo kwa baadhi ya mechi kwenye kwenye Ligi Kuu Bara au Ligi ya Championship.

Ukiwa mbali na familia ya soka unaweza kudhani suala hili haliwezekani, lakini ukiwa karibu hasa na wale wanaojiita 'watu wa mpira' utagundua soka hasa la Tanzania lina mambo mengi sana katika nyuma ya pazia.

Ukienda nyuma ya pazia utaambiwa mambo mengi sana ya kushangaza kuhusu rushwa kwa waamuzi, na hata wachezaji kwa ajili ya kucheza chini ya kiwango ili kuzifungisha timu zao na kunufaisha upande wa pili. Wenyewe wachezaji wanasema mchezaji huwa hashuki daraja, ni klabu ndio inashuka, hivyo baadhi yao wala hawaoni hasara kuchukua fedha kutoka sehemu nyingine na kuifungisha timu yake.

Kwa bahati mbaya sana, kile kinachozungumzwa nyuma ya pazia, huwa hakizungumzwi na mtu yoyote anayekuja jukwaani.

Nina maana wanamichezo wengi wanajua mengi kuhusu shughuli za kupanga matokeo inavyofanyika, nani anahusika, ukitaka ushinde mechi yako uende kwa nani, fedha zitapelekwa vipi, lakini hilo katu huwezi kuona linazungumzwa kwenye vyombo vya habari, au pale inapopaswa kuzungumzwa.

Sababu ni nyingi, inawezekana ikawa ni ile ile ya siku zote. Suala la rushwa ni gumu mno kulithibitisha kwa sababu huwa ni kwa mtoaji na mpokeaji tu wenye kuthibitisha tukio hilo.

Nyingine ni sababu za kisiasa, mtu anaweza kuwa na nia nzuri ya kutaka kukomesha jambo hilo, lakini wakati analipeleka kwenye mamlaka, kabla halijafika kwa wahusika akakutana na lundo la vizingiti , ikiwamo yeye mwenyewe kugeuziwa kibao.

Lakini niseme tu kama jambo hili litafuatiliwa kwa umakini na kwa dhati kabisa bila kuweka urafiki, woga na siasa pembeni, tunaweza kuona ambayo hatukutarajia kuyaona.

Mwaka 2016 nchi ilitikisika kutokana na timu nne za Geita Gold ambayo kwa sasa ipo Ligi Kuu, Polisi Tabora, JKT Kanembwa na JKT Oljoro kupatikana na hatia ya kupanga matokeo ya kwenye mechi za mwisho za Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara sasa Ligi ya Championship, ambapo mbali na baadhi ya viongozi kufungiwa, lakini klabu hizo ziliteremshwa daraja.

Uamuzi huo ulitoa ujumbe katika ligi zetu baadhi ya mechi kuwapo na mchezo mchafu.

Hivi sasa Fountain Gate FC inayoshiriki Ligi ya Championship imepeleka barua kwa Bodi ya Ligi juu ya rushwa, ikihituhumu Kitayosce ya Tabora kuwahonga baadhi ya wachezaji wake ili wacheze chini ya kiwango.

Barua hiyo iliwasilishwa katika Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi hiyo, Fountain Gate inamtuhumu mmoja wa makocha wake ambaye kwa sasa wameshamtimua, pamoja na mmoja wa viongozi wa Kitayosce kufanya mbinu chafu ya kuwashawishi baadhi ya wachezaji wao kupanga matokeo.

Katika barua hiyo ambayo wameambatanisha na ushahidi wa sauti na picha, wamelalamika Aprili 28, mwaka huu, siku moja kabla ya mechi iliyowakutanisha, viongozi hao walifanya mbinu chafu za kuwashawishi baadhi ya wachezaji wa Fountain Gate kupanga matokeo kwa kuwatumia fedha.

Huu ni ujasiri wa hali ya juu na wanapaswa kupongezwa. Matokeo yoyote yatakayokuja, lakini viongozi wa Fountain Gate wameonyesha wapo vizuri kutaka kupambana kuondoka tabia ya rushwa michezoni kwa vitendo na kukusanya ushahidi na kupeleka kunakohusika bila woga, badala ya kulalamika na kusema mara nyingi jambo hili halina ushahidi.

Kilichofanyika na viongozi hao ni uchunguzi kwa kutumia vifaa na itelejensia, ambapo imezishinda hata timu zenye uwezo wa kifedha na rasilimali watu ambao wanaweza kutengeneza mfumo wa kubaini timu yao kuhujumiwa, na kuupeleka ushahidi kunakohusika, lakini zimeshindwa kufanya hivyo.

Kwa vyovyote itakavyokuwa hili ni somo zuri kwa klabu nyingine za hapa nchini kutokaa kinyonge na kulalamika, zifuate nyayo za Fountain Gate, kwa sababu ikishajulikana hivyo, klabu au viongozi wenye tabia hiyo wataanza kuingiwa na woga na kuacha hujuma hizo.




Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Schreiner, akizungumza katika kongamano la maadhimisho ya Siku ya Wakunga Duniani, lililofanyika Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA.**

# Serikali yawatoa hofu wananchi kuhusu uuzaji hisa Tanga Cement

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI imewatoa hofu Watanzania kuhusu uuzaji wa hisa za Tanga Cement ikisema kiwanda kinachozalisha bidhaa aina ya Simba hakitafungwa wala kufa, huku ikisisitiza mchakato unaoendelea umefuata sheria na taratibu.

Imesema Tanga Cement kwa sasa inahitaji msaada na 'inapumulia mashine' kujiendesha kutokana na kuwa na deni la Sh. bilioni 203, urari wa kifedha una nakisi ya Sh. bilioni 11 wakati matumizi yaliyozidi kiwango (overdraft) ni zaidi ya Sh. bilioni 219.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (pichani), aliyasema hayo jana bungeni wakati akijibu hoja za wabunge kuhusu mchakato wa ununuzi wa hisa za Tanga Cement.



"Serikali imepeleka macho mawili katika suala hili kwa sababu kuna maslahi ya taifa. Kampuni ya Afriscam ndiyo yenye hisa nyingi asilimia 69. Zilizobakia zinamilikiwa na serikali kupitia mifuko ya hifadhi ya jamii. Kwa hiyo niwatoe hofu wabunge na Watanzania kiwanda hakiwezi kufa," alisema.

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, wakati akihitimisha pamoja na kujibu hoja za wabunge kutokana na hotuba ya makadirio ya wizara kwa mwaka 2023/24, alisema wabunge na Watanzania wafahamu kwamba Tume ya Ushindani (FCC) haikushughulika na ombi la muunganiko wa kampuni ya Tanga Cement na Twiga Cement.

"Hoja ya wabunge kwa nini FCC iliruhusu mchakato huu wa muungano wakati awali ilizuiwa na Tume ya Ushindani wa Kibiashara (FCT). Jibu sahihi ni kwamba FCC haikushughulika na ombi la muungano wa kampuni hizo," alisema.

Waziri Kijaji anasema Desemba 22, mwaka jana, kampuni ya Scancern International DA ambayo ni kampuni tanzu ya Heldelbeg Cement AG inayomiliki asilimia 69 Twiga Cement iliwasilisha ombi la kununua hisa za asilimia 68 za Kampuni ya Afrisam ndani ya Kampuni ya Tanga Cement.

"Taratibu zote za kisheria zilifuatwa za kuwasilisha na kuchambua ombi hilo. Kwa mujibu wa Kifungu cha 11, Kifungu Kidogo cha 2 cha Sheria ya Ushindani kinachosomeka sambamba na Kanuni ya 33 ya kanuni za ushindani za mwaka 2018 na Kanuni ya 2 ya Kanuni ya kwanza ya kizingiti cha kuomba kuunganisha kampuni za mwaka 2017 kinatoa wajibu kwa kampuni zinazotaka kuungana na zimekidhi vigezo vya vifungu hivyo kuwasilisha maombi yao pasipo kujali kusudio lao la awali lilikubaliwa au lilikataliwa," alisema Kijaji

Kijaji alisema ombi lililoruhusiwa ni ombi jipya kulingana na vifungu tajwa kwa kumbukumbu ya barua iliyopokelewa serikalini yenye namba CBC 127359/144. Alisema ombi hilo lilipokewa mwaka 2022 na kwamba wizara haikuwa na haja ya kutumia tamwimu za mwaka 2011.

"Natamani sana Watanzania watuelewe, ombi hili jipya lililoruhusiwa na FCC ni tofauti na lile la awali la namba CBC 127359/136 lililowasilishwa Novemba 2, 2021 ambalo lilitumia tamwimu za Desemba 2020," alisema.

Dk. Kijaji alisema ombi hilo liliruhusiwa kwa masharti Aprili 6, 2022 kwa kuzingatia kigezo cha uwezo uliosimikwa.

"Tuliruhusu kwa sababu utawala wa soko wa kampuni zilizoomba kujiunga kutumia Installed capacity (kigezo (kilichowekwa) ilikuwa inafikia asilimia 31.53 ambazo ni chini ya asilimia 35 ya mwisho kuruhusiwa kwa kampuni," alisema.

Alisema sheria haijasema itumike kigezo kilichowekwa kiasi cha mauzo kwa sababu Sheria ya FCC ni sheria ya kiuchumi ambayo inajihusisha na tabia za wateja wake wa eneo lile walilopo, kwamba inabadilika wakati kwa wakati.

Kuhusu hoja kwamba hakukuwa na uwazi wakati wa ununuzi wa hisa za Tanga Cement, Kijaji alisema baada ya ombi kuletwa FCC, tangazo liliwekwa katika magazeti ya serikali Januari 11, mwaka huu, kwamba hakukua na malalamiko yoyote.

Alisema taasisi ya kutetea walaji, wadau wa kuzalisha saruji walishiriki na walilidhika kuendelea kwa mchakato huo, hawakupinga.

"Huyo anayekuja kinyumenyume nani? Anayepinga ni nani? siri yake nini? Kwa nini asiseme adhima yake, aseme ili tujue," alisema Kijaji.

# Mbunge aingia bungeni na pombe kali

**Na Gwamaka Alipipi**, DODOMA

MBUNGE wa Momba (CCM), Condester Sichalwe, ameingia bungeni akiwa na pombe kali, akiitaka serikali kuwasaidia wabunifu wa pombe za kienyeji kufanya utafiti na kuzifungasha vizuri ili kupata soko.

Sichalwe alizishika pembe hizo na kumwonyesha Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, wakati akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka 2023/24.

"Viwanda vinaanza na mtu wa chini wa kawaida. Tuheshimu mawazo yanayotolewa na Watanzania wenzetu, wanatengeneza K-Vant. TBS (Shirika la Viwango Tanzania) wanaenda kupima bandarini lakini kwenda kukaa na kushirikiana na watu wa chini wawasaidie hawaendi," alisema.

Mbunge huyo aliitaka serikali iwatumie wabunifu wa pombe wakiwamo ambao wamekuwa wakitengeneza vinywaji vinavyokaa siku tatu kwa kuwasaidia kuziboresha ili kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja.

"Najiuliza kwa nini pombe za gongo zinamwagwa. Ubunifu si unaanza na wazo? Ndiyo maana wanatengeneza gongo kwa nini wasipewe usaidizi wa ubunifu, kwani ubunifu unataka ni nini?" alihoji.

Alisema athari inayotajwa katika gongo ni ethanol na methanol lakini wako wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ambao wamefanya utafiti na kugundua hakuna madhara makubwa.

"Kumekuwa na kasumba kubwa ya kuingiza kila kitu kutoka nje, itafikia mahali tutaingiza hadi dhambi. Uingizaji wa pombe serikali yetu hatuna dini ila wananchi ndiyo wanaamini dini," alisema.

Alisema kuna pombe inauzwa nchini kwa Sh. 270,000 wakati kuna wajasiriamali wanaouza pombe aina ya gongo lakini wanakamatwa badala ya kupewa elimu ya kuendeleza pombe hiyo.

Hoja hiyo iliombewa taarifa na Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenan, ambaye alisema pamoja na uzuri wa hizo chupa hizo za pombe hata watumaji wengi hawajui imetengenezwa na kitu gani, lakini hizo (pombe) za Watanzania zinafahamika rasilimali zake zimetoka wapi.

Baada ya taarifa hiyo, Sichalwe aliendelea kusema: "Kule kijijini kuna pombe nyingi za kinyeji kama vile chimpumu, gongo huu ndiyo ubunifu. Kinachozuiliwa kwenye gongo ni methanol."

Hata hivyo, Mbunge wa Viti Maalum, Agnes Hokororo, aliomba taarifa akisema: "Wakati wakulima wa korosho wanalalamikia bei ndogo ya korosho ghafi, matunda ya korosho yaani mabibo yana uwezo wa kutengeneza pombe bora, lakini huo ubunifu haujatumika vizuri."

Baada ya taarifa hiyo, sichalwe aliendelea kusema aliwasiliana na wataalamu kutoka UDSM, wakamweleza kuwa walishafanya utafiti kwenye pombe aina ya gongo na kubaini kwamba haina madhara.

# Walalamikia ubovu miundombinu stendi mpya

**Alex Sayi,** MASWA

MIUNDOMBINU ya Stendi mpya ya Maswa iliyopo katika Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, inayotumiwa na magari zaidi ya 70 kwa siku, imelalamikiwa kuwa ni mibovu kwa muda mrefu na kuchangia uharibifu wa vyombo vya usafiri vinavyoingia hapo.

Hivi karibuni Nipashe ilitembelea stendi hiyo na kubaini uchakavu wa miundombinu ya barabara, vyoo, uchafu wa mazingira pamoja na uwapo wa nyasi ndefu zinazoonekana kutokatwa kwa muda mrefu.

Mwenyekiti wa Umoja wa Mawakala wa Usafirishaji, Hassan Bunango, akizungumza na gazeti hili alisema kuwa licha ya halmashauri kuendelea kukusanya ushuru wa Sh.3,000 kwa kila gari linaloingia hapo, lakini hakuna ukarabati wowote uliofanyika.

"Kero hii ni ya muda mrefu na viongozi wa halmashauri tulishawaambia lakini hatuoni kinachoendelea. Vyoo ni chakavu, barabara za kuingilia ni mbovu. Kwa hali hii hatuoni faida ya sisi kulipa ushuru," alisema.

Alisema licha ya awali kukubaliana barabara hiyo iwekwe molamu lakini mpaka sasa hakuna utekelezaji.

Alisema stendi hiyo kila siku imekuwa ikitumiwa na magari zaidi ya 70 na kila moja hulipa Sh.3,000, ikiwa ni zaidi ya Sh. milioni 75 kwa mwaka.

Mwenyekiti Kitongoji cha Stendi Mpya, Abrazack Msuya, alisema amekuwa akilazimika kukaa vikao na umoja huo kwa lengo la kuwahamasisha pamoja na wafanyabiashara kujitolea kufweka nyasi na kufanya usafi ili kuweka mazingira safi.

"Nimekuwa nikitumia mfumo wa Ulaghibishi kwenye Kitongaji changu, ninawashirikisha wadau waone umuhimu wa kuwajibika badala yakulalamika kwa kusubiri serikali," alisema Msuya.

Mtendaji wa wa Mamlaka ya Mji Mdogo Maswa, Saimon Nyadwera alisema stendi hiyo bado ipo kwenye maboresho hivyo wanatakiwa kuendelea kuwa wavumilivu wakati marekebisho yakifanyika.

Kuhusu suala la usafi alisema ni wajibu wa kila Mtanzania kuhakikisha anasafisha na hakuna sababu ya kulalamika kwa kisingizio cha kulipa ushuru.

"Kama kuna watu wanajitolea kufanya usafi ni jambo jema lakini eneo hili ni kubwa na tayari tuna watu wa kufanya usafi licha ya kuwa wachache kulinganisha na ukubwa wa eneo lenyewe," alisema.

Ofisa Afya wa Wilaya, Budodi Walwa, alisema kuwa uwapo wa nyasi hizo unatokana na wamiliki wavibanda kushindwa kufanya usafi kwenye maeneo yao kama utaratibu unavyoelekeza.



Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Kigoma, Laurent Kabikiye (kulia), akiwasilisha mada kwenye kikao kazi cha mkakati wa kutokomeza vipimo batili maarufu kama bidoo kwenye biashara ya Mawese, wakati wa kikao kilichohudhuriwa na viongozi wa mkoa huo jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wanawake Masasi wahimizwa kusajili biashara

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imewataka wanawake wajasiriamali wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kusajili kampuni na majina ya biashara ili kutambulika kisheria.

Rai hiyo ilitolewa na Msaidizi wa Usajili wa BRELA, Suleiman Suleiman, wakati akitoa elimu kwa wanawake wajasiriamali 110 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Masasi iliyofanyika Aprili 29, mwaka huu, wilayani humo.

Suleiman alisema pamoja na changamoto wanayokumbana nayo wajasiriamali wengi katika kutumia mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao, BRELA iko tayari wakati wote kutoa usaidizi hivyo wanapokwama wasisite kuwasiliana na BRELA kupitia kituo cha miito ya simu ili kupatiwa usaidizi.

Alisema BRELA imekuwa ikitoa elimu kwa wadau mbalimbali wakiwamo wajasiriamali ili kuhakikisha kuwa wadau wote wananufaika kutokana na sajili pamoja na leseni zinazotolewa na BRELA.

"Kuna manufaa mengi ambayo mnaweze kupata kutokana na kurasimisha biashara zenu kwani mbali na kulindwa kisheria pia kuna fursa za kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha pamoja kupata zabuni mbalimbali serikalini", anafafanua Suleiman.

Msadizi wa Usajili wa BRELA, Athuman Makuka, aliwaelimisha wanawake hao umuhimu wa kuwa na alama za biashara katika bidhaa zao ili ziweze kutambulika.

Alisema watakaposajili alama za biashara itakuwa rahisi kwa bidhaa zao kujitofautisha na nyingine, hivyo kuwa na uhakika na soko la bidhaa zao na kwamba usajili pia utamuwezesha mjasiriamali kupata haki ya kipekee ya alama ya biashara au huduma.

Hali hiyo, alisema itasaidia kuzuia wengine kutumia alama yake sokoni ili kujipatia manufaa kinyume na sheria lakini pia itamuwezesha mjasiriamali kuhimili soko la ushindani kwakuwa itakuwa ni rahisi wateja kutambua bidhaa yake sokoni.

Ofisa Leseni wa BRELA, Jubilate Muro, aliwasihi wajasiriamali kusajili viwanda vidogo BRELA kwani katika wilaya hiyo wengi wao wana viwanda vidogo vya kubangua korosho, kutengeneza sabuni na batiki ambavyo kisheria vinapaswa kusajiliwa.

Awali, akifungua mafunzo hayo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mtwara, Agnes Hokororo, alishukuru jitihada zinazofanywa na BRELA kuwafikia wadau mahali walipo na kuwapatia elimu.

Hokororo alisema kwakuwa wanawake wengi wilayani humo wamejikita katika sekta isiyo rasmi ili waweze kujikomboa kiuchumi, mafunzo haya yamefika wakati mwafaka kwa kuwa watanufaika na kuwa mabalozi wa kufikisha elimu ya BRELA kwa wengine.

Hokororo alikiri kuwa wajasiriamali wengi wilayani humo hawajasajili majina ya biashara hivyo elimu ya BRELA itawawezesha kufuata utaratibu wa kusajili majina ya biashara.

Wanawake wajasiriamali wa Halmashauri hiyo wamepatiwa elimu kuhusu Usajili wa Majina ya Biashara na Kampuni, Alama za Biashara na Huduma na jinsi ya kupata leseni za biashara na viwanda.

# WMA yatekeleza agizo la Waziri Mkuu Kigoma

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Vipimo (WMA), imeendelea kutekeleza agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, la kuhamasisha kilimo cha mchikichi alipofanya ziara mkoani humo.

Katika ziara hiyo aliyoifanya mwaka jana, Waziri Mkuu aliagiza kutokomezwa kwa vipimo batili maarufu kama 'bidoo' kwenye biashara ya mawese kwa kuwa vinawapunja wakulima wa zao hilo.

Katika utekelezaji wa agizo hilo, WMA imefanya kikao na viongozi mbalimbali wa mkoa wa Kigoma na katika ufunguzi wa kikao hicho, mgeni rasmi, Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe, Kanali Michael Ngayalina, alisema ni kweli kwamba matumizi ya vipimo na udhibiti wake, hususani kwenye biashara ya mawese umekuwa na changamoto nyingi.

Alitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni kukosekana kwa masoko na vituo rasmi vya kufanyia biashara ya mawese kwenye maeneo mengi, hali inayotoa mwanga kwa wanunuzi kununua mawese kwenye vinu vya uzalishaji na wakati mwingine kwenye nyumba za wananchi (wakulima).

"Hali hii si tu kwamba inafanya kazi ya udhibiti wa matumizi ya vipimo kuwa ngumu, bali huikosesha serikali (mamlaka zetu) sehemu ya ushuru pamoja na kushindwa kupata takwimu sahihi za uzalishaji na mauzo ya mawese," alisema.

Ngayalina aliipongeza WMA kwa kuendelea kusimamia matumizi ya vipimo kwenye maeneo mbalimbali ya biashara na huduma pamoja hatua walizokwisha chukua kufikia sasa kudhibiti matumizi ya vipimo batili kwenye biashara ya mawese kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema lazima wahakikishe biashara hiyo inafanyika kwa haki na usawa bila upande wowote kupunjika na aliitaka WMA kusaidia upatikanaji wa vipimo vya gharama nafuu ambavyo vitatumika kupimiwa mafuta ya mawese.

Meneja wa WMA Mkoa wa Kigoma, Laurent Kabikiye, alisema wakala inatoa elimu mara kwa mara kuhusu madhara ya kutumia vipimo batili (bidoo) ili kumlinda mkulima wa zao la chikichi na mnunuzi pia.

"Pamoja na elimu hiyo wakala wa vipimo inafanya jitihada za kutafuta vipimo vitakavyo patikana kwa gharama nafuu ambavyo vitakuwa na ujazo mbalimbali ili kuwasaidia wafanyabiashara wa mawese kuuza bidhaa zao kwa kutumia kipimo hicho ambacho ni sahihi ili kuwasaidia kupata faida bila kupunjwa," alisema.

Katika kikao hicho ambacho kilihudhuriwa na viongozi na watendaji mbalimbali wa mkoa wa Kigoma wakiwamo wakuu wa wilaya za mkoa, makatibu tawala wasaidizi sekretarieti ya mkoa, makatibu tawala wa wilaya, wakurugenzi watendaji wa halmashauri za mkoa, maofisa tarafa, maafisa biashara kutoka halmashauri zote za mMkoa, mameneja wa SIDO na TBS na watumishi wa WMA.

Washiriki wa kikao kazi hicho kwa pamoja walikubaliana kuwa halmashauri zianzishe masoko ya kuuzia na kununulia mawese pamoja na kununua vipimo vilivyohakikiwa na WMA na kuhamasisha wauzaji wa mawese kununua vipimo ili vitumike kununua na kuuzia mawese na kutokomeza matumizi ya bidoo.



# Bosi wa Magereza ageukia mazingira

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMISHNA Jenerali wa Magereza, Mzee Nyamka, amewaagiza maofisa, askari na watumishi kutekeleza agizo la serikali la kupanda miti ya matunda na aina zingine maeneo ya jeshi hilo ili kutunza mazingira.

Akizungumza jana kwenye upandaji miti ya matunda na mbao kwenye eneo la makao makuu ya jeshi hilo Msalato jijini Dodoma, iliyotolewa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), alisema jeshi hilo limetakiwa kupanda miti milioni 1.5 nchi nzima.

Nyamka alisema hadi sasa takwimu zinaonyesha tayari wamepanda miti 850,000 katika maeneo mbalimbali ya jeshi hilo.

"Tunaona jinsi miti ilivyo na faida kwenye utunzaji wa mazingira kwa sababu Dodoma ya sasa huwezi kuilinganisha na Dodoma ya miaka ya 1980 na 1990 kutokana na miti inayopandwa imechangia kubadilisha mazingira,"alisema.

Mkuu huyo aliwahimiza maofisa na askari wa jeshi hilo kuhakikisha kila mmoja katika eneo lake anapanda miti ya matunda, mbao na aina zingine za miti ambazo huleta faida kwenye suala la mazingira.

"Naomba kila mmoja ahakikishe katika eneo lake anapanda mti uwe wa matunda au kivuli,lengo ni kuunga mkono jitihada za serikali za kutunza mazingira yetu," alisema.

Awali, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Salum Omary, alisema upandaji wa miti wanashirikiana na TFS pamoja na Mfuko wa Misitu Tanzania (TAF),ambao wametoa miti ya matunda pamoja na mbao.

Alisema ushirikiano huo unaleta matokeo chanya katika utunzaji wa mazingira kama serikali inavyoelekeza utaratibu wa upandaji miti ufanyike katika kila eneo.

Omary alisema ushirikiano wao na TFS unasaidia baadhi yao kwenda kupata mafunzo ya utunzaji misitu na miti katika Jeshi la Magereza.

Naye Naibu Kamishna wa Utawala na Rasilimali watu wa jeshi hilo, Jeremia Katungu, alisema lengo la upandaji miti hiyo katika maeneo ya ndani ya Magereza na nje ni kuhakikisha wanaikijanisha nchi pamoja na maeneo hayo ili kutunza mazingira.

Alisema miti iliyopandwa katika makao makuu ya jeshi hilo ni ya mbao na miembe ambayo itasaidia kupata matunda lakini pia ya mbao ikistawi itavunwa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kiuchumi za jeshi hilo.

Katungu alisema mpango wa upandaji miti ni endelevu ili kuunga mkono jitihada za serikali za kuhakikisha wanaikijanisha nchi pamoja na kutunza mazingira.

# Walia uhaba huduma za matibabu

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

WAKAZI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kibaigwa wilayani Kongwa, wameomba serikali kuboresha huduma za kijamii ikiwamo upatikanaji wa dawa ili wananchi wapate huduma bora za matibabu.

Ombi hilo lilitolewa na wakazi hao jana kwa Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel, kwenye mkutano wa hadhara wa wananchi uliofanyika Kibaigwa.

Mmoja wa wananchi hao, Yohana Makavu, alisema kuwa Kituo cha Afya cha Kibaigwa hivi sasa kimeelemewa na kushindwa kutoa huduma za afya ipasavyo.

Alisema kwa wagonjwa wenye bima ya afya wanapofika kupata matibabu huambiwa wakanunue dawa katika duka ya dawa badala ya kupewa kituoni hapo.

"Tunaiomba serikali kuwapunguzia makali ya changamoto zilizopo kwenye sekta ya afya, elimu na miundombinu zinazogusa jamii," alisema.

Akijibu hoja kuhusiana na upatikanaji wa dawa katika kituo hicho kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Wilaya, Katibu wa Afya, Abdallah Missenye, alisema serikali imeruhusu kuwapo kwa maduka ya dawa ya jamii ili kuboresha huduma za upatikanaji wa dawa.

Hata hivyo jibu hilo halikukubaliwa na wananchi hao.

Naye Mkuu wa Wilaya hiyo, Remedius Emmanuel alisema serikali itaendelea kutatua kero zinazowakabili wananchi huku akiwataka kuzingatia sheria katika utekelezaji wa shughuli zao ikiwa ni pamoja na kutojihusisha na biashara za magendo.

"Serikali haitomfumbia macho mtu yeyote atakayebainika kujihusisha na biashara haramu zikiwamo dawa za kulevya, siku za hivi karibuni Jeshi la Polisi Wilayani Kongwa lilipokamata magunia 98 ya mahindi ya serikali yakiingizwa katika soko la Kibaigwa kwa njia za magendo,"alisema.



Mbunge wa Momba, Condesta Sichwale akionyesha aina mbalimbali za pombe kali za kisasa, wakati akichangia hotuba ya makadirio na mapato ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, bungeni jijini Dodoma jana. Mbunge huyo, aliomba pombe kali za kienyeji kupewa vibali ili ziuzwe kwenye maduka ya vinywaji. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Rai yatolewa kuanzishwa mifuko elimu mamlaka serikali za mitaa

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

SERIKALI imeombwa kuanzisha mfuko wa elimu katika kila halmashauri ili kusimamia ubora wa elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi isiyo ya kiserikali ya Professor Mwera Foundation, Hezbon Mwera, alitoa rai hiyo juzi kwenye mkutano wa wadau wa elimu mkoa wa Singida wa Mwaka 2023.

Alisema mfuko huo utasaidia kuweka sawa ubora wa elimu pia kusaidia vijana wenye uhitaji ndani ya halmashauri zao.

"Vilevile wazazi wana jukumu la kuhakikisha mwanafunzi anapata chakula kipindi anachokuwepo shuleni ili kumfanya azidi kuelewa kwa kuwa baadhi hushindwa kufanya vizuri kutokana na njaa," alisema.

Alishauri jamii kuwapeleka katika vyuo vya ufundi wanafunzi waliomaliza au wanaosubiria matokeo ya kidato cha nne na darasa la saba ili kusomea kozi za muda mfupi ambazo zitawasaidia kuongeza utaalamu.

Aidha, alisema vijana wakisoma kozi za muda mfupi zitawaongezea sifa mbalimbali katika utendaji kazi wao katika miaka ya baadae.

Mkurugenzi huyo alisema mpaka sasa wamewasaidia zaidi ya vijana 3,500 na Sh. bilioni tatu zimetumika kupata elimu ya ufundi bure bila malipo kutoka Mwaka 2019 mpaka sasa kupitia Chuo cha Ufundi Tarime kinachomilikiwa na taasisi hiyo.

Alisema wanawasaidia pia watoto yatima ambao wanaishi katika mazingira magumu kuanzia elimu msingi sekondari pamoja na vyuo vya ufundi.

"Tuna fursa ya kusaidia wale wanaotoka katika mazingira magumu ili waweze kufikia malengo, maisha haya tunaishi kwa ajili ya binadamu wenzetu, mipango tunayoweka hatuwezi kufanikiwa pasipo kupitia kwa binadamu wenzetu," alisema.





# Zanzibar kujenga Bandari Kizimkazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kuongeza huduma za usafirishaji bahari, serikali ya Zanzibar imedhamiria kujenga bandari ya Kizimkazi, Kusini Unguja pamoja na Wete ambazo zitavifungua kiuchumi visiwa hivyo na mikoa jirani ya Tanzania Bara ukiwamo Tanga.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Khalid Salum Mohamed, wakati akishuhudia utiaji saini wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu ya utekelezaji wa miradi miwili ya ujenzi wa bandari katika visiwa hivyo.

Alisema kuwapo kwa bandari ya Kizimkazi ni muhimu kwa ajili ya kuongeza shughuli za usafiri kati ya wananchi wa vijiji jirani katika mkoa huo ambao wamekuwa wakifanya safari kwenda Tanzania Bara.

Pia alisema serikali imechukua jukumu hilo ikiwa ni sehemu ya mikakati yake ya kuongeza shughuli za kibiashara kwa wananchi wa pande mbili hizo ili kupata kipato cha uchumi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Shomari Omar Shomari, alisema upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya Wete ni muhimu ambao utasaidia kwa kiasi kikubwa katika kukifungua kisiwa cha Pemba na mikoa jirani ya Tanzania Bara ikiwamo, Tanga hadi Mombasa nchini Kenya.

Alisema ziko shughuli nyingi za kibiashara katika kisiwa cha Pemba na mikoa jirani ikiwamo Tanga na Mombasa na kwamba ujenzi wa bandari ni muhimu katika kichocheo cha mapato na ukuaji wa uchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Harbour Engineering Cheng, Yong Jian, alisema wamejipanga kufanya kazi hiyo kwa uadilifu mkubwa na kutumia utaalamu pamoja na kuwasilisha kazi hiyo kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa wakati kwa utekelezaji.

Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar, alisema wakati umefika kwa serikali kukifungua Kisiwa cha Pemba kiuchumi na uwekezaji.

# Wauguzi wahimizwa kujiendeleza kielimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, amesema misaada ya vifaa tiba inayotolewa kwa ajili ya hospitali na vyuo vya afya Zanzibar, haitakuwa na tija iwapo wauguzi hawako tayari kujiendeleza kielimu katika ngazi za juu.

Akizindua maabara na vifaa vipya vya kufundishia wanafunzi wa kuzalisha na kuhudumia mama na watoto kisayansi katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Kitivo cha Uuguzi Mbweni visiwani humo, Mazrui alisema neno ahsante pekee halitoshi bali vitendo ndivyo vinavyotakiwa.

Msaada huo umetolewa na jumuiya inatotoa huduma za kiafya Zanzibar (WAJAMAMA) kwa kushirikiana na taasisi za 'Ariadne Labs' na Laedral kutoka Marekani zinazoshughulikia huduma za afya ya uzazi na mtoto.

"Hawa waliotusaidia hawakuja kutuambia iko siku watatuletea bali wameonyesha vitendo, hivyo nanyi mwonyeshe shukrani kwa kusoma vizuri na baadaye mkafanye kazi nzuri katika vituo vya afya," alisisitiza.

Mazrui alisema lazima wanafunzi wa fani ya uuguzi, udaktari na kada nyingine za afya, wachangamkie fursa za kutafuta elimu ya juu, wasome na kusomesha ili Zanzibar iwe na nguvu kazi nzuri na ya kutosha hasa upande wa afya ya uzazi.

Waziri huyo alisema serikali inaendelea kujenga hospitali za kisasa za wilaya na mikoa lakini kikwazo kikubwa ni uhaba mkubwa wa wauguzi wenye shahada ya kwanza kuendelea.

"Wauguzi wengi tulio nao ni wenye stashahada. Vijana wengi wanaotaka kazi hujielekeza zaidi kwenye uhudumu (Ordelies) na kutandika vitanda. Mahodari mnaowajua nyinyi wa kizamani hatuwataki sasa, tunahitaji waliosomea kazi hiyo na wakipewa nafasi wanawajibika kitaalamu," alisema. Alisema hivi karibuni Wizara ya Afya ilitangaza nafasi 195 za kuanzia kwa wauguzi wenye stashahada na walijitokeza karibu 400 na upande wa shahada kati ya nafasi 150 zilizotangazwa walipatikana 42.

Pia alisema wizara ilitangaza nafasi 20 za madaktari bingwa lakini kwa bahati mbaya pamoja na kubembeleza wamepatikana wanne hali inayoonesha vijana hawataki kusoma.

Mazrui aliishukuru WAJAMAMA na washirika wake kwa msaada wao ambao alisema umegusa eneo muhimu la afya ya uzazi yenye changamoto kubwa ya vifo vingi vya mama na watoto visiwani humo.

Akitoa takwimu za vifo, Waziri Mazrui alisema mwaka 2021/22, wanawake 50 na watoto 1,363 walipoteza maisha na kuanzia Julai, mwaka jana hadi Machi, mwaka huu, vifo vya watoto ni 1,567 na wanawake 46 viliripotiwa.

Mwanzilishi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa WAJAMAMA, Nafisa Jiddawi, alisema sambamba na vifaa walivyotoa, pia wamefundisha walimu 56 watakaosomesha wanafunzi.

"Vifaa na matengenezo haya ikiwamo watu na watoto bandia kwa ajili ya kujifunzia kuzalisha na kuhudumia kwa njia ya kisasa vimetugharimu Sh. milioni 500. Vinahitaji mazoezi mengi ili wauguzi wanapofanya kazi wodini wawe wameiva na kuepuka makosa yanayoweza kuleta madhara kwa mgonjwa,"alisema.

Mkurugenzi wa Ushauri katika Taasisi ya Ariadne Lab, Dk. Amber Weiseth, na Meneja Utekelezaji kutoka Laerdal Global Health-Tanzania, Dk. Grace Qorro, walisema dhamira yao ni kuendelea kuunga mkono serikali ya Zanzibar katika juhudi zake za kuimarisha sekta ya afya.

Walikihakikishia chuo hicho kwamba msaada huo hautaishia hapo, bali watafuatilia na kutoa miongozo kwa walimu na wanafunzi wa uuguzi kila itakapohitajika.

Mwenyekiti wa Baraza la Wauguzi na Wakunga Zanzibar, Prof. Amina Abdulkadir, alisema hatua ya WAJAMAMA inaakisi ndoto za kuiona Zanzibar siku moja inapata Chuo Kikuu maalum cha uuguzi kilichosheheni vifaa bora na walimu waliobobea kitaaluma.

Naibu Makamu Mkuu wa chuo hicho-Taaluma, Ali M. Ussi, alisema maendeleo ya taifa lolote duniani yanahitaji nguvu kazi yenye afya ambayo inatengenezwa kwa ushirikiano chini ya usimamizi wa taasisi zenye dhamana.



Mkuu wa idara ya maendeleo ya jamii Manispaa ya Shinyanga, John Tesha, akigawa vifaa vya shule kwa watoto wanaoishi mitaani na walioacha masomo kwa sababu mbalimbali na kisha kuwarudisha kuishi na wazazi wao ili waendelee na masomo na kutimiza ndoto zao, hivi karibuni. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Sera maendeleo ya vijana yakamilika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, amesema rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ambayo lengo lake kubwa ni kuliwezesha kundi hilo kujitegemea na kuendeleza miradi ambayo itaongeza ajira, imekamilika.

Akizungumza jana visiwani Unguja kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025 pamoja na mpango kazi wa bajeti ya nusu mwaka, Waziri Mwita alisema itahusisha uimarishaji wa baraza la vijana.

Pia alisema sera itahusisha majukumu yake ya kuliendeleza kundi hilo ambapo jumla ya vijana 2,132 wanatarajiwa kufikiwa kwa kuibua miradi ya uchumi na uzalishaji mali ambayo itazalisha ajira.

Alisema iko miradi ambayo vijana wanatakiwa kuibuwa kwa ajili ya utekelezaji wake na hivyo kujiajiri katika sekta binafsi.

Katibu Baraza la Vijana Zanzibar, Salum Issa Makame, alisema marekebisho ya sera hiyo ni muhimu kwa kuwa, yatasaidia kuwapo kwa ushirikishaji mkubwa wa baraza la vijana kwa wananchi wengi wa makundi tofauti.

Hata hivyo, alisema bado kuna mwamko mdogo wa vijana kujiunga kwenye mabaraza ya vijana na kusababisha kundi hilo kushindwa kushirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ambayo itawapatia ajira. Katibu wa Idara ya Itikadi na Uenezi ya CCM Zanzibar, Mbeto Khamis Mbeto, alisema wizara hiyo ni tegemeo katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi katika masuala ya ajira kwa vijana.

Alisema ni wakati mwafaka kwa wizara pamoja na baraza la vijana kulishajihisha kundi hilo kuhakikisha wanajiunga katika mabaraza ili kupata ufumbuzi tatizo la ajira.



**AYRA**
UKURASA 14



JUMAMOSI MEI 6, 2023



# KUNA SIKU MTAELEWA TU

USIKU wa kuamkia Aprili 30 mwaka huu kwenye Ukumbi wa The Super Dome, Masaki, Dar es Salaam walipatikana washindi wa tuzo za muziki Tanzania (TMA) zilizoandaliwa na Baraza la Sanaa la Taifa.

Wasanii wengi maarufu nchini walijizolea tuzo hizo, ambapo sitoweza kuwataja wote, lakini kwa uchache nikiwataja wale maarufu zaidi ni Diamond Platnumz, Rayvanny, Harmonize, Zuchu, Billnas, Dulla Makabilla, Sholo Mwamba, na wengine wengi.

Hata hivyo, kabla ya tuzo zenyewe, kuna baadhi ya wasanii waliibuka na kuzisusia kwa sababu ambazo wanazifahamu wenyewe.

Baadhi yao ni Dully Sykes na Mbosso ambao wao waliweka bayana kuwa hawakubaliani na jinsi baadhi ya wasanii kuwekwa kwenye vipengele siyo, lakini pia kuna malalamiko ya baadhi ya ngoma kutochaguliwa kuingizwa kwenye vipengele vya mashindani.

Dully yeye akasema wazi kuwa wamuondoe kwenye kipengele cha tuzo, si kwa ubaya, ila alishakataa kushirikishwa kwenye tuzo hizi tangu zamani.

Akadai kushangazwa kuwekwa kwenye tuzo wakati yeye alishazitakaa, hivyo moja kwa moja inaonekana hazitaki na ameshazisusia.

Mwingine ni Mbosso ambaye yeye alishusha lundo la malalamiko akidai mara nyingi tuzo hizi hulenfa kuwatunza watu ambao makati inaweza kuwamudi, kuwaendesha na kuwatumia watakavyo na siyo waliofanya vizuri kiukweli kwenye mwaka husika.

Basata ilitolewa ufafanuzi hizo. Jambo la msingi hapa ni kwamba inaonekana kuna wasanii wana woga wa kushindwa. Kwenye pambano lolote mtu akionyesha woga wa kushindwa mapema si mshindani mzuri.

Kilichotakiwa ni kuacha tu kiendelee kwa sababu wanaochagua wimbo wa msanii fulani wanafanya hivyo kwa sababu wanaona umefanya vema, ndiyo maana wanauingiza kwenye mashindano.

Nadhani msanii yoyote anayeingizwa kwenye kinyang'anyoiro, hata kama watashindwa, lakini jina lake bado linabaki, na pia anakuwa ameheshimika kwa kitendo tu cha ngoma yake kuchaguliwa kwenye mashindano, kwani nyingi zimechwa.

Kuhusu baadhi ya nyimbo zilizoonekana 'zimehiti' lakini hazikuingizwa, hiyo ipo dunia nzima. Ni muhimu watu wakaheshimu maamuzi wa waandaaji na wahusika. Hata kwenye kuchagua wachezaji wa timu za taifa dunia nzima, mashabiki huwa hawarishiki.

Hii isiwakatishe tamaa Tanzania Music Awards na Basata, kama mtu hakuelewa sasa, kuna siku ataelewa tu.

BASI SAWA

## Marioo kafa kaozaa

PENZI zito kati ya mwanamuziki wa Bongo Fleva, Marioo na mrembo Paula ambaye ni mtoto wa mwigizaji Kajala Masanja, linazidi kuchanua na sasa kila kitu kinaanikwa hadharani.



Wawili hao ambao walianza kama mchezo, lakini kila kukicha mambo yanazidi kunawiri na Paula anaonekana kufurahia uhusiano huo.

Marioo alimnyakua Paula miezi kadhaa baada ya kuvunja uhusiano wake na msanii mwingine, Rayvanny ambaye amerudisha majeshi kwa mama mtoto wake, Fahyvanny.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Marioo alipakia video ya Paula akinengua kiuno kwa taratibu na kusema kwamba hicho ni chakula chake anachokiona na kinamtamanisha mara kwa mara.

## Quiz Life kutoka kiafrika zaidi

Msanii anayekuja kwa kasi kwenye Bongo Fleva, Maige Mtondi, maarufu kama Quiz Life amesema endapo atapata mtu wa kusaidia kazi zake anaamini atatangaza vyema asili na tamaduni za kiafrika.

Akizungumza na BT, Quiz Life, anayetamba na wimbo 'Nesesa', amesema tangu mwaka 2019



amekuwa akifanya muziki kwa kujisimamia mwenyewe jambo linalofanya achelewe kutimiza ndoto zake.

"Ukiangalia kwa wasanii wapya ambao wanakuja hakuna anayenifikia kwa ubunifu hasa katika kuitangaza Tanzania na tamaduni za kiafrika jambo ambalo linaniangusha ni kukosa meneja anayeweza kuwekeza kwenye kipaji changu, naamini nikipata muwekezaji nitafanikisha lengo langu ndani ya mwaka huu,," amesema Quiz.

Aidha msanii huyo ametamba kuwa licha a kutokuwa na meneja lakini ameweza kufanya harakati zake za muziki huku akihimili viwango vya ubunifu na mwonekano eake kama wasanii wakubwa.



## NAVVY KENZO KUMVUTA RICK ROSS

WANAMUZIKI wanaounda kundi la Navy Kenzo, wiki hii wamejikuta wana bahati baada ya kupiga stori na rapa maarufu wa Marekani Rick Ross, ambaye alionekana kuvutiwa na kazi zao.

Kutokana na maongezi yao katika Insta Stori, kuna uwezekano wasanii hao wakafanya ngoma ya

Sip n Whine iliyoimbwa na Aika wa Navy Kenzo

Kama mipango hiyo itakamilika Navy Kenzo watakuwa wamekwenda mbali kutokana na rapa huyo maarufu kuwa katika ndoto ya wasanii wengi wa Afrika.



## Wema na pombe, hapana kabisa

MWIGIZAJI mkongwe wa filamu za Bongo. Wema Sepetu ametangaza rasmi kuwa hajagusa kinywaji chochote chenye kilevi kwa muda wa miezi mitano.

Akizungumza mara baada ya kukutana na mtangazaji mbwatukaji wa Clouds, Mwijaku Burton, Wema amesema baada ya kuacha kunywa pombe ameanza kunawiri kiasi ambacho kwa sasa ana mwonekano wa kupendeza.

"Nina miezi mitano tangu niache kutumia pombe, si unaona vile niko vizuri nimependeza," Wema amesema huku akitoa tabasamu pana.

FILAMU

## Too Late: Mchawi hafiki mbali

**Na Adam Fungamwango**

HAKUNA methali au msemo wa wahenga ambao ulisemwa bila ya kuwa na uhalisia. Kwa sababu wao walifanya tafiti, ingawa si za kitaalam, lakini zile za kuishi kwenye jamii wakagundua vitu vingi sana vinavyoendelea hadi karne ya sasa.

Kuna methali isemayo,' kikulacho ki nguoni mwako', 'mchawi ndugu', ' anayekumulika mchana usiku atakuchoma', 'wazuri hao na wabaya ni hao hao', na zingine nyingi.

Maana ya methali hizi zote ni moja tu. Kuwa siku zote ukipatwa na jambo lolote baya, basi atayekuwa amekufanyia hivyo ni mtu wa karibu sana kwako. Ni mtu anayefahamu nyendo zako na kila kitu. Waliona mtu asiyekufahamu hawezi kukufanyia ubaya. Wakagundua hata mtu wa nje, au asiyekufahamu, akitaka kumfanyia mtu ubaya ni lazima amshirikishe anayemfahamu kiundani.

Hili pia limepatikana kwenye filamu inayoitwa 'Too Late', au 'Umechelewa.' Fuatilia kwa makini utakubaliana na hili.

Pad na rafiki yake Jeff ni wasanii wa bongo fleva ambao bado 'hawajatoka' na lengo lao baadaye wawe wasanii wakubwa.

Wanaishi kwenye chumba kimoja, lakini anayekilipia ni Pad. Pad anabahatika kumpata msichana aitwaye Aisha, mtoto wa uswazi.

Lakini siku si nyingi anampata mwingine aitwaye Amina. Huyu ni ushuani mambo safi. Msichana huyu ilifika wakati akawa anampa pesa Pad. Alikuwa anamiliki wasichana wote wawili kwa wakati mmoja, Hata hivyo cha ajabu ni kwamba akienda kwa demu mmoja, mwingine anakuwa anajua. Akitoka kwa huyu, mwingine anafahamu kuwa ametoka kwa mwanamke mwingine. Tena na majina wanafahamiana. Hii ilikuwa inamchanganya mno Pad. Kuna wakati alidhani kuwa huenda wale wanawake wawili ni mmoja na ni jini linalojibadilisha.

Haiwezekani akienda kwa Amina, akitoka huko Aisha anamwambia kila kitu na alichokuwa akikifanya.

"Mwambie huyo demu wako, siku nikikutana naye ama zake ama zangu." Aisha alipiga mkwara.

"Wewe una mwanamke mwingine, hapa unanidanganya tu, sasa ni lazima uchague moja, mimi au yeye." Hayo ni maneno ya Amina.

Kuna siku Amina alimpa kadi kwenda kutoa pesa kwenye ATM akiwa na rafiki yake Jeff, lakini cha ajabu ni kwamba muda mfupi baadaye Aisha alifika na kumnyang'anya Pad pesa, pamoja na kadi aliyopewa na mpenzi wake mpya.

Hali ikawa mbaya. Pad akawa hajui nini kinaendelea. Mwisho wa siku alikuja kugundua kuwa rafiki yake Jeff ndiye anayefanya yote hayo.

Ndiye anayefanya mawasiliano na wanawake wote wawili, kila mmoja akijulishwa Pad anachofanya na mwingine.

Amina ndiye alivujisha siri hiyo baada ya kuhakikishiwa kuwa sasa ameamua kuwa naye yeye pekee.

Aliporudi nyumbani alimkuta rafiki yake Jeff akimhadithia Aisha anafanya hayo yote kwa sababu anampenda sana Amina, na anataka amuachanishe, rafiki yake abaki na Aisha, yeye amchukue Amina.

Pad anachoamua anamtimua Jeff, pamoja na Aisha. Maamuzi yake ni kwamba sasa atabaki na Amina tu.

## BENDI 5 ZILIZOTOKA MGONGONI

**Na Adam Fungamwango**

MASHABIKI wa muziki wa dansi wanazifahamu bendi mbalimbali za zamani na kisasa na wamekuwa wakizishabikia nyimbo zao na wanamuziki wao, lakini si wengi wanaofahamu asili ya kuanzishwa kwake.

Kuna bendi zilianzishwa kwa ajili ya wazo tu la watu fulani, lakini zipo zilizoanzishwa kwa mgongo wa bendi zingine.

Yaani kuna bendi zilizokuwepo mwanzo ambazo kwa sababu mbalimbali tofauti zimesababisha kuundwa kwa bendi zingine.

Wakati mwingine zote zinakuwa maarufu au ilioanzishwa baadaye inakuwa maarufu zaidi. Lakini zipo ambazo zinasababisha iliyosababisha kuundwa kwa nyingine kupungua nguvu na kufa.

Hapa leo tutaziangalia bendi mbalimbali maarufu sana nchini, au za Watanzania waliokuwa wakiishi nje ya nchi ambazo zilianzishwa kwa mgongo wa nyingine.

**Msondo Ngoma/ Kilwa Jazz**

Si wengi wanaofahamu kuwa msingi wa kuundwa kwa bendi ya NUTA Jazz ni Kilwa Jazz. Bendi ya Kilwa Jazz ilikuwepo kabla ya Uhuru, ikiongozwa na Ahmed Kipande. Na ndiyo ilitumbuiza siku ya Uhuru wa Tanganyika. Ikawa ndiyo bendi pendwa nchini. Ilikuwa ikitumbuiza kwenye sherehe zote za kichana na kiserikali. Mwaka 1963, miaka miwili baada ya Uhuru ilitumbuiza kwenye sherehe za Siku ya Wafanyakazi, Mei Mosi. Kilwa Jazz walifanya vema sana, kiasi cha kuwatamanisha viongozi wakuu wa Chama Cha Wafanyakazi wakati huo kuunda bendi hao. Walinunua vyombo na kuchukua wanamuziki kutoka bendi mbalimbali na mara ya kwanza chama hicho kilichoitwa NUTA wakati huo kikawa na bendi yao na kutumbuza kwa mara ya kwanza Mei Mosi mwaka 1964. NUTA Jazz, ndiyo baadaye ikawa Juwata Jazz, Ottu Jazz, na baadaye Msondo Ngoma Music Band.

**DDC Mlimani Park/Dar International**

DDC Mlimani Park, maarufu kama Sikinde Ngoma ya Ukae ni hasimu mkubwa wa Msondo Ngoma. Ilianzishwa kwa mgongo wa Dar International. Asilimia 99 ya wanamuziki wa bendi hiyo ndiyo waliounda Orchestra Mlimani Park. Dar International iliundwa mwaka 1977, wanamuziki wake wengi wakitokea Safari Trippers. Mwaka 1978 ulitokea mgogoro kwenye bendi hiyo. Walichofanya ni kuviacha vyombo na wanamuziki wake kwenda sehemu nyingine kuunda Sikinde mwaka 1978. Walimuongeza Muhidini Maalim Gurumo kutoka Juwata Jazz bendi ikaanza, ingawa baadaye walichukua na wengine Msondo, akiwemo Hassan Rehani Bitchuka kwaka 1979.

**Super Volcano/Morogoro Jazz**

Super Volcano ni bendi iliundwa na Mbaraka Mwinshehe mwaka 1973, akijiengua kutoka Morogoro Jazz. Alichukua karibuni asilimia 90 ya wanamuziki wa Morogoro Jazz, hivyo Super Volcano imetoka kwenye mgongo wa bendi ya Morogoro Jazz.

**TK Limpopo/Cuban Marimba**

Kama Mbaraka alivyofanya, Juma Kilaza naye mwaka 1973 alijiengua na bendi ya Cuban Marimba na kuunda ya kwake, akaita TK Limpopo, naye vile vile akisomba wanamuziki kutoka bendi yake ya zamani, akiwemo Hemed Maneti.

**Les Wanyika/Simba Wanyika**

Les Wanyika iliundwa mwishoni mwa miaka ya 1970 na asilimia zaidi ya 90 ya wanamuziki wa Kitanzania, ikiwa na makao yao nchini Kenya. Asili ya bendi hii ni Simba Wanyika. Ina maana imeundwa kwenye mgongo wa Simba Wanyika ya Willson Peter Kinyonga na George Peter.

Kulitokea kutoelewana kati ya Willson na wanamuziki wake, wakaamua kumuacha na kwenda kuunda bendi nyingine wakaiita Les Wanyika. Hata mdogo wa Willson, George alitaka kujiunga nao na kumuacha kaka yake, lakini wanamuziki waliojiengua walimkataa, akaenda kuunda Orchestra Jobiso ingawa baadaye akarejea kwa kaka yake.



# Ayra ataka kuwa Rihanna

MWIGIZAJI maarufu wa Nigeria, kutoka lebo ya Mavin, Ayra Starr ameeleza kuwa na ndoto ya kushirikiana na nyota wa muziki wa Marekani, Rihanna.

Msanii huyo ameeleza kuwa amekuwa akimtazama Rihanna kama mfano wake kwa sababu alikua akimsikiliza na kumchukulia kama malkia.

Amemsifia Rihanna kwa kuongeza uwezo wa kujiamini na amekuwa akimpenda msanii huyo kwa miaka yote.



## Iyanya hiyo kama fiksi

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Onoyom Mbuk, anayejulikana kwa jina la Iyanya, amefichua undani wa kukutana kwake na shabiki kwenye tamasha la Davido.

Awali, Iyanya akitumia ukurasa wake wa Twitter, alikiri kuvutiwa na mwanamke alipokuwa akitumbuiza hafla iliyofanyika TBS. Ndani ya saa 24, mwanamke huyo alipatikana na kuunganishwa na mwimbaji huyo.

Baadhi ya fununu zilisambaa kuwa mwanamke huyo alikuwa mpenzi wake wa siri.

Iyanya katika tangazo lake, amesema alikuwa akimpa tabasamu mwanamke huyo kutokana na kuwa na mfadhaiko uliotokana na ndugu yake kuugua saratani.

## Mwombeeni Jamie Foxx

MCHEZA Filamu maarufu kutoka Hollywood, Jamie Foxx, bado anaendelea kupigania uhai wake hospitalini zaidi ya wiki 3, imeelezwa kwa sasa kinachohitajika ni maombi pekee.

Foxx amelazwa hospitalini baada ya matatizo ya kiafya, lakini familia yake haijasema nini kinachomsumbua.

Hata hivyo, wandani wa familia hiyo wamesema mashabiki wake wanatakiwa kufanya maombi ili miujiza ya Mungu ifanyike kumrejesha katika hali yake ya kawaida.

Aprili 12, binti yake Foxx, Corinne, alitangaza kuwa baba yake alipata matatizo ya kiafya na kusababisha kukimbizwa hospitalini kwa ajili ya matibabu.

Jamie pia ni mtangazaji wa kipindi maarufu cha muziki cha "Beat Shazam" katika runinga ya FOX, ambacho kilikuwa kikiandaliwa kabla ya kuugua.





## Genevieve Nnaji arudi tena

MWIGIZAJI Mkongwe kutoka Nollywood, Genevieve Nnaji, amejitokeza hadharani baada ya kutojihusisha na mitandao ya kijamii kwa miezi mingi.

Nnaji ameibuka katika mtandao wa Twitter wakati akiadhimisha miaka 44 ya kuzaliwa kwake juzi.


Alichapisha picha yake mpya na kuandika 'Plus One'huku kushiriki salamu alizopewa kutoka kwa marafiki zake, wakiwemo Waje, Stella Damasus, Uche Jombo, Funke Akindele, na Ini Edo.

## Dada wa Burna boy apagawa

RONAMI Ogulu, ambaye ni dada wa mwimbaji maarufu wa Nigeria, Burna Boy, amesema amefurahishwa na kaka yake kushiriki tamasha la Met Gala ya 2023.

Hafla hiyo ya kila mwaka, ambayo ilitoa heshima kwa mbunifu wa mitindo marehemu Karl Lagerfeld, ilifanyika Mei 1, katika jumba la makumbusho la Metropolitan na kuvutia wageni wengi mashuhuri kutoka duniani kote.

Mavazi ya Burna Boy katika ukumbi wa Met Gala yamepokewa vizuri kutoka kwa wapenda mitindo na mashabiki, huku wengi wakimpongeza kwa kuvaa nguo inayovutia na maridadi.








Mwenyekiti wa Jumuiya ya Tawala za Mikoa (ALAT) Mkoa wa Manyara, Peter Sulle (katikati), akizungumza wakati akifungua kikao cha ALAT cha kujadili maendeleo na changamoto za halmashauri saba za mkoa huo, katika Mji mdogo wa Katesh, wilayani Hanang' juzi. Kushoto ni Katibu wa ALAT Mkoa huo, Anna Mbogo na Makamu Mwenyekiti, Baraka Kanunga. **PICHA: GIFT THADEY**

# Gwajima asisitiza malezi ya vijana kuokoa taifa mmomonyoko maadili

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewasihi viongozi wa umma kuacha kulala usingizi, badala yake watimize jukumu lao la kuwafunda vijana maadili mema ili kuokoa kizazi kijacho.

Dk. Gwajjima alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na baadhi ya viongozi wa mkoa wa Arusha walioshiriki mafunzo ya maadili ya viongozi wa umma yaliyoandaliwa na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

"Lazima sisi viongozi tuwe mstari wa mbele kuwafundisha maadili mema vijana wetu ili kuwaepusha kudumbukia kwenye vitendo vinavyokinzana na maadili yetu ukiwamo ushoga na mapenzi ya jinsia moja.

"Tujiulize tunafanya nini kujenga kizazi bora katika taifa letu, lazima tuzingatie maadili yetu. Ajenda ya maadili sio ya utumishi wa umma au nyinyi viongozi peke yenu, ni ajenda ya wananchi wote," alisema.

Awali, akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Arusha, David Lyamongi, alielekeza wakuu wote wa taasisi za umma kuzingatia maadili ya utumishi wa umma wanapotimiza majukumu yao ili kujenga imani ya serikali kwa wananchi na kuwasaidia wananchi kunufaika na rasilimali za nchi.

"Maadili ya kiongozi wa umma yanatakiwa kujidhihilisha mahali popote, kiongozi wa umma anapokuwa ofisini, mtaani au ndani ya familia yake, lazima awe mfano kwa jamii iliyomzunguka," alisema.

Lyamongi pia aliagiza watendaji wakuu katika taasisi mbalimbali za Mkoa huo, kutoa miongozo mbalimbali inayohusu masuala ya utumishi kwa watumishi walioko chini yao ili iwasaidia kujua mabadiliko ya kiutumishi.

"Ni vizuri mkatoa miongozo inayotolewa na Serikali kuhusu mabadiliko mbalimbali yakiwemo maslahi ya watumishi ili kuwasaidia watumishi kujua mabadiliko husika katika utumishi wa umma," alisema.

Naye Katibu Msaidizi kutoka Makao Makuu ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fabian Pokela, alisema miradi ya taifa ya kimkakati kutosimamiwa vizuri kunatokana na baadhi ya viongozi wanaohusika na miradi hiyo kukosa uadilifu.

## Tatizo barabara Same ni historia

**Na Mary Mosha,** SAME

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amesema serikali imemaliza tatizo la mawasiliano ya barabara, kati ya wakazi wa Same Mashariki na Same Magharibi baada ya kukamilisha ujenzi wa daraja la mawe.

Jana, Babu alisema kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na matengezo ya barabara kwan kiwango cha changarawe, urefu wa kilomita 3.5 katika barabara ya Ndungu/Makokane.

"Sote ni mashahidi, adha ambazo tumepata kabla ya kujengwa kwa daraja hili, ikiwemo watu kupoteza maisha, watoto kushindwa kwenda shule na wajawazito na wagonjwa kupoteza maisha. "Tulitunze, wasitokee watu kufanya ubadhilifu kwenye miundombinu nasi tukawanyamazia, tutoe taarifa za kina na tuwe walinzi. Kwa sasa, tunaamini mazao yatafika sokoni bila mkulima kuteseka, tulime kwa wingi na tupate faida na kukuza uchumi wa nchi," alisema.

Kabla ya kujengwa daraja hilo, vijana wanne walikufa maji baada ya kwa kusombwa na maji katika eneo hilo.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) wa Wilaya ya Same, James Mnene, alisema daraja hilo lilianza kujengwa mwaka 2021/22, alisema daraja hilo la mawe lenye urefu wa mita 36, limeigharimu serikali Sh. milioni 200 zilizotokana na fedha za tozo.

Mmoja wa wakazi wa Ndungu, Mohamed Issa, akieleza furaha yake baada ya kukamilika kwa daraja hilo, alisema awali daraja hilo lilikuwa hatari kwa maisha ya wananchi.

"Awali nyakati za mvua, wananchi tulikuwa hatuwezi kupita kutokana na wembamba wa daraja hili na kujaa maji hadi kupita juu. Binafsi nimewahi kushashudia watu wanne wakiwa wamepoteza maisha kutokana na kusombwa na maji hapa hapa," alisema.

# EAC yatumia ardhi kiduchu uzalishaji chakula

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MTANDAO wa Wakulima Wadogo wa Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAFF), umefichua siri kuwa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hazitumii asilimia 70 ya ardhi kwa ajili ya shughuli ya uzalishaji wa chakula.

Kwa mujibu wa Kiongozi wa Shirika la Association of Women in Agriculture in Kenya (AWAK), Julius Mundia, asilimia 30 pekee ya ardhi, ndiyo inayotumiwa na wakulima kwa uzalishaji wa chakula.

Mundia alikuwa akizungumza jana jijini hapa wakati akichokoza mada kwenye kongamano la kwanza la Jumuiya ya Asasi za Kiraia za Afrika Mashariki linaloendelea.

"Kutokana na data (takwimu) tulizochukua kutoka mashirika mbalimbali ikiwamo Umoja wa Mataifa (UN), Shirika la Kilimo na Chakula (FAO) na Benki ya Dunia (WB), tumegundua ya kwamba suala la ardhi inayofaa na inayotumika kwa sasa kuzalisha chakula, tunatumia asilimia 30 katika nchi zote saba za EAC, huku asilimia 70 ikiwa haitumiki."alisema.

Alisema kutokana na kiwango kikubwa cha ardhi kutokutumika kwa shughuli za kilimo nchi hizo, zinakabiliwa na uhaba wa upatikanaji wa chakula na chakula kinachopatikana hakitoshelezi mahitaji ya wananchi wake.

"Tunaposema kuhusu usalama wa chakula tunatakiwa kutumia rasilimali ya ardhi hata kama ni kutegemea mvua tunapaswa kulima ardhi yote ili kupata chakula cha kutosha na kingine kitakachobaki tunaweza kuunza nje ya ukanda wan chi za EAC," alisisitiza Mundia.

Pia alisema Jumuiya ya Afrika Mashariki inapaswa kuweka mpango mkakati wa kuhakikisha kuwa maeneo yote ambayo hayajalimwa wayatumie kwa kilimo ili kuwapo na chakula cha kutosha na kukabiliana na baa la njaa kwa baadhi ya nchi hizo.

Naye Mkuu wa Idara ya Kilimo na Usalama wa Chakula kutoka EAC, Fahari Marwa, alisema jumuiya hiyo inasaidia nchi wanachama katika mambo mbalimbali ikiwamo kuweka miongozo ya pamoja,sera na sheria ambazo zitasaidia kukuza sekta ya kilimo.

"Tumekuwa tukitoa miongozo ambayo inaelekeza ni jinsi gani nchi wanachama wanaweza kukabiliana na matatizo mbalimbali katika sekta ya kilimo ikiwamo mabadiliko ya tabianchi.

"Tuna miongozo ya usajili wa viuatilifu,pia tuna sheria ya mbegu na mbolea hivyo sheria,miongozo na taratibu zikifuatwa tunaweza kufikia malengo yaliyowekwa,"alisema.

Mwenyekiti wa ESAFF, Bailraine Hakim, alisema mkutano huo umewakutanisha wakulima wadogo kutoka mashariki na kusini mwa Afrika kujadiliana na kuangalia namna nchi hizo zitaweza kuweka mipango ya kuongeza fedha kwenye kilimo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Wakati, Mwenyekiti wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), Apolo Chamwela, alipingana na utafiti huo akisema ardhi kubwa inatumiwa na wakulima wakubwa badala ya wadogo.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kuruka kamba mchezo ulioteka mabinti na watoto enzi hizo

- Ulipunguza unene, kuwapa muonekano wa kuvutia
- Wimbo 'Aziza' wa Msondo uliotumika

Na Adam Fungamwango

AZIZA sasa naomba, turudiane, hayo yamekwisha, kipenzi changu, shetani katupitia, rudi mke wangu eee, mimi mwenzio mama ninapata tabu."

Ni kipande wa wimbo wa bendi ya Juwata Jazz, iliyokuwa inatumia mtindo wake wa enzi na enzi, Msondo Ngoma unaitwa 'Aziza.'

Wimbo ulikuwa maarufu sana kuanzia mwaka 1977 na ndizo zilikuwa moja kati ya nyimbo za mwanzo za bendi hiyo baada ya kubadilisha jina kutoka Nuta Jazz kuja Juwata jazz.

Mbali na kupendwa kama moja ya nyimbo kali na zilizofanya vizuri na 'kuhiti' sana wakati huo, ambapo kila kona unayokata unaweza kuusikia redioni au mtu anauimba.

Kikubwa zaidi ni kwamba wimbo huu, bila watu kukaa kikao, au kupiga kura, au kutoa maagizo, ulitumika na watoto na wasichana kwenye mchezo wa kamba ambao ulikuwa maarufu sana wakati huo.

Haukuwa mchezo hasa wa wavulana, badala yao wao walikuwa wanavutiwa tu wakiona watoto au wasichana wakicheza, hivyo nao walikuwa wakijisogeza kwenda kutazama kama vile mashabiki wanavyoangalia mpira wa miguu au ngumi.

Haukutofautiana na 'rede', kwani wasichana wawili wanakuwa wameshika kamba na mmoja atakuwa yupo kati anaruka. Kinachotakiwa ni kwamba ile kamba ipite juu ya kichwa cha mtu wa kati na miguu yake chini. Kitendo cha kushindwa kufanya hivyo atakiwa amekosea.

Mchezo huo uliambatana na nyimbo mbalimbali, zilizotungwa au kuchukuliwa kutoka sehemu nyingine baada ya kuonekana zinafaa kuingizwa kwenye mwendo wa urukaji kamba.

Wimbo husika ulichaguliwa na mchezaji mwenyewe, anayeruka kati, huku wenzake wanaorusha wakimuitikia au kumsindikiza. Akikosea kwa kushindwa kuruka na yeye anakwenda kushika kamba, mmoja anaingia kati.

'Aziza' ndiyo ulikuwa wimbo maarufu zaidi wa kamba miaka hiyo na hakuna mwanamke yoyote mtu mzima kwa sasa aliyekuwa anacheza mchezo huo akawa haujui. Wewe waulize tu. Muulize mama, shangazi, mama mkubwa au mdogo, atakwambia.

Kulikuwa na nyimbo nyingi sana, baadhi yao ni huu.

"Shilingi ya Nyerere katikati kuna mwenge. Doli doli, doli samwela." Nao pia ulitumia kwenye mchezo wa kuruka kamba.

Kuna wimbo mmoja mrefu, ambao mchezaji ni lazima awe na pumzi, unaimbwa hivi.

"Mosi kibanda chafuka moshi, pili macho kama pilipili, tatu bwana mchonga viatu, nne tumpate tumchune, tano bizari ya manjano, sita, Waarabu waenda vita, saba ndiyo siku ya mahaba, nane zunguka tuagane, tisa fungueni madirisha, kumi kwa matete na mangumi."

Acha huo kuna nyimbo zingine zilikuwa fupi tu ambazo hazikumpa tabu mchezaji, hasa yule ambaye hana pumzi za kutosha.

"Matikiti kudondoka, kudondokea, kudondoka, kudondokea." Halafu kuna ule wa. "Ukitaka tende chukua, hata halua chukua, lakini kidogo amua, lakini kidogo amua."

Hizi ni baadhi ya nyimbo chache tu zilizotamba sana kwenye michezo huo ya kuruka kamba hasa kwa akinadada wakati huo, na lengo, pamoja na umoja, urafiki na mshikamano, lakini ni mazoezi tosha yaliyoyafanya kulinda miili yao kiafya na shepu zao, kuepuka madhara ya kunenepa ovyo wakiwa na umri mdogo.



Kuruka kamba ilikuwa ni kama njia ya kuwapa miili yao mazoezi mepesi ambayo yaliyowapa utimamu wa mwili, afya njema bila gharama ya kwenda 'gym' na kulipa pesa nyingi kama ilivyokuwa sasa.

Faida nyingine kwa mujibu wa wataalam ni kuchoma kiasi kikubwa cha mafuta mwilini hasa kwenye maeneo yenye mrundikano wa mafuta kama vile tumbo, makalio, mapaja, mikono, shingoni na mashavuni.

Hii iliwafanya wasichana wengi wa miaka ya nyuma miili yao kutoathiriwa zaidi na unene uliokithiri, au kuonekana kuwa na umri mkubwa na kuzeeka mapema kabla ya umri halisi waliokuwa nao. Badala yake wengi walionekana bado wanadai, wakati umri wao umekwenda kutokana miili yao kuwa na mazoezi ya kutosha.

Kwa sasa mchezo huo ambao wakati huo ulichezwa kila kona, hasa nyakati za jioni, umepotea na badala yake baadhi ya wasichana ambao wanataka kudhibiti unene wa miili yao, wanalazimika kwenda vituo vya kufanyia mazoezi na kulipa pesa nyingi.

Na wale ambao hawafanyi mazoezi athali zake kwa sasa zinaonekana bayana, wasichana wengi wa sasa wamekuwa na miili mikubwa usiyoendana na umri wao, na tayari limeanza kuja tatizo lingine la vitambi kwao. Vyakula wanavyokula sasa vingi ni vya mafuta, lakini pia hawana mazoezi kama yale ya zamani, hasa michezo, ikiwemo kuruka kamba.

Je, kuna nyimbo zingine za kuruka kamba enzi zile ambazo unazifahamu?

**Tuma meseji 0716 350534**



# Dar wahadharishwa magonjwa mlipuko

**Na Joseph Mwendapole**

WAKAZI wa mkoa wa Dar es Salaam wamepewa tahadhari dhidi ya mlipuko wa kipindupindu kwa kuhakikisha maeneo yao yanakuwa safi muda wote.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, alisema hayo jana wakati wa kongamano la kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuhusu ugonjwa huo.

Alisema mwaka 2012 ulifanyika utafiti na kubaini kwamba duniani kote watu karibu bilioni 1.8 huwa wanaugua magonjwa yanayotokana na uchafu kama kipindupindu.

Kiwango hicho, alisema ni sawa na asilimia 28 ya watu wote duniani wanaougua magonjwa yanayoendana na uchafu kama kuharisha, kutapika na maradhi ya tumbo kwa ujumla.

Dk. Mfaume alisema iwapo wananchi watazingatia kanuni za afya kama kunawa mikono kabla ya kula, watajiepusha na magonjwa mbalimbali kama kuharisha na kutapika.

"Mara nyingi kunapotokea ugonjwa wa mlipuko jamii inakuwa na taharuki kwa hiyo tumeona ni vyema tuwaite hapa tuwape taarifa kuna wagonjwa wangapi na hatua mbalimbali ambazo serikali inachukua kukabiliana nao," alisema.

Kwa mujibu wa Dk, Mfaume, wagonjwa waliohisiwa wakati wa mlipuko huo walikuwa 15 lakini mpaka sasa kwenye vituo vya huduma vya afya hali ni nzuri kwa kuwa wengi wamesharuhusiwa na kuondoka.

Alisema asilimia 90 ya vifo vinavyotokana na wagonjwa wanaoharisha na kutapika kunatokana na matumizi ya maji yasiyo safi na salama na kwamba ndiyo sababu wameishirikisha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

Dk. Mfaume alisema mamlaka hiyo imeendelea kutibu maji kwenye matenki mbalimbali mkoa wa Dar es Salaam na kutoa vidonge vya kutibu maji vya chlorine kuanzia ngazi ya kaya.

Alisema serikali inaendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara wenye visima vya maji ili wahakikishe wanayaweka kwenye mazingira salama kabla ya kuyapeleka kwa wananchi.

"Unapopata mgonjwa anayeharisha na kutapika mpe huduma ya kwanza kwa kumpa maji kwasababu anapoharisha anapoteza maji kwa wingi kisha muwahishe hospitalini kwasababu huwezi kujua kama ni kipindupindu au ugonjwa gani, usimweke nyumbani muda mrefu" alisema.

Ofisa Afya Mkoa wa Dar es Salaam, Enezael Ayo, alisema taarifa ya kuanza kwa mlipuko wa ugonjwa wa Kipindupindu ilitolewa tarehe 20 mwezi uliopita ambapo kulikuwa na watu 15 waliohisiwa kuwa na ugonjwa huo.

Alisema mpaka sasa watu hao 15 wameruhusiwa na kwa sasa hakuna aliyelazwa na kwamba sampuni 13 zilikusanywa kwa ajili ya kupimwa Maabara Kuu ya Taifa ya Afya ya Jamii na sampuli saba zilikuwa na vimelea vya ugonjwa wa Kipindupindu.

"Kati ya watu waliohisiwa kuwa na ugonjwa huo, tisa walikuwa wanawake na uchambuzi wa wagonjwa wa Kipindupindu kwa sehemu ulionyesha kuwa wagonjwa 13 walitoka Wilaya ya Ilala ambao ni sawa na asilimia 86.7," alisema.

Alisema hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Mkoa kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo ni pamoja na ukaguzi wa majengo, masoko na kaya kuangalia usafi wa mazingira na usafi.

Mkoa una dawati la kupokea taarifa za magonjwa kutoka kwa jamii na vituo vya afya, ufuatiliaji wa wanaohisiwa kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa kipindupindu unaendelea na kuendelea na ukusanyaji wa sampuli za maji kutoka kwenye visima na maji.

Alisema serikali inaendelea kutoa elimu ya afya kwa jamii kwa kutumia wataalamu wa afya wa Kata na ili kuongeza uelewa na ufuatiliaji.

## Mradi umeme Rusumo wakamilika asilimia 99

**Na Restuta James**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema mradi wa kufua umeme kwa njia ya maji Rusumo, umekamilika kwa asilimia 99.

Taarifa iliyotolewa na TANESCO jana ilisema kuwa ujenzi wa jengo la mitambo ya kufua nishati hiyo, njia ya kusafirisha umeme ya kilovoti 220, kituo cha kupokea, kukuza na kusafirisha umeme na nyumba za wafanyakazi umekamilika.

"Mradi wa Rusumo unatekelezwa kwa ushirikiano wa nchi tatu za Tanzania, Rwanda na Burundi. Mradi una jumla ya megawati 80 ambapo kila nchi itapata megawati 27.

Kukamilika kwa mradi wa Rusumo kutaimarisha gridi ya taifa upande wa kaskazini magharibi mwa Tanzania ambayo ni Mikoa ya Geita, Kagera na Kigoma," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kukamilika kwa mradi wa Rusumo kunaelezwa kutaongeza uhakika wa umeme katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuufanya mkoa wa Kagera kuanza kutumia umeme wa gridi ya taifa.

Aidha, mgawo huo wa megawati 27 utaongeza uwezo, nguvu na uhakika wa umeme katika mikoa hiyo na kwenye gridi ya taifa.

Mradi huo umehusisha ujenzi wa mtambo wa uzalishaji umeme, bwawa, eneo la kupokea umeme kabla haujasambazwa na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kutoka eneo la mradi hadi Nyakanazi.



Kijana Swai Kidevu akiwahudumia wateja wake wa mbuzi choma katika baa mpya ya Fest Point katika kijiji cha Mkanyangeni, wilayani Muheza, mkoani Tanga jana. Baa hiyo yenye ukumbi na nyumba ya kulala wageni imetoa ajira kwa vijana zaidi ya 30 wa kijijini hapo. Wa (pili kushoto) ni Mwekezaji Patrick Kisaka. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Bosi TARURA apewa siku 90 kujitathmini

**Na Anthony Gervas,** MAGU

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, wamempa siku 90 Meneja wa Wakala Barabara Mijini na Vijijini(TARURA), Mhandisi Nyonyoli Wawa, kutoa ufafanuzi kuhusu miradi ya barabara kujengwa chini ya kiwango.

Hatua hiyo ilifikiwa juzi na madiwani hao katika kikao kilichofanyika mjini hapa baada ya kuibuka hoja na malalamiko mengi kuhusu wakala kuwa haifanyi kazi vizuri katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususani barabara.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mpandalume Simon, alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ametoa zaidi ya Sh. bilioni mbili katika mwaka wa fedha 2022/23 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo lakini utekelezaji wake ni wa viwango duni.

Simon alizitaja barabara zilizojengwa chini ya kiwango kuwa ni pamoja na Ilungu, Kisabo- Rangi, Mwamanga,Sayaka hadi Bugatu na Chandulu - Nkungulu ambazo zimeharibika kwa muda mfupi na haziwezi kupitika, hivyo kusababisha changamoto kwa wananchi.

Alisema kimsingi TARURA wilayani Magu imekuwa haifanyi kazi vizuri, hivyo kuwatia wasiwasi madiwani.

Alisema pamoja na kwamba iko chini ya usimamizi wa serikali kuu, lakini miradi ya maendeleo ipo kwa wananchi wao.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, wamempa meneja huyo matazamio ya miezi mitatu wakimtaka kikao kinachofuata cha robo ya nne kitakachofanyika Julai, mwaka huu, afike akiwa na taarifa zote za utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na matumizi ya fedha. Tyofauti na hivyo, alisema ataondolewa katika wilaya hiyo.

Alisema maoni ya madiwani ni kutaka kumfukuza kufanya kazi kwa kuwa amekosa nidhamu ikiwamo uhusiano na ushirikiano mbovu na viongozi wengine, jambo linalosababisha kuibua hoja na malalamiko mengi ya kutoridhishwa na utendaji kazi wake.

Kutokana na mwenendo wake huo, alisema madiwani wamemtaka kujitathimini mapema kabla mambo hayajaharibika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LIZBETH SHAYO** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI mali ya **ONE ACRE FUND** yenye namba za usajili **T 126 CYL.** Chasis Namba: **AHTFR22G106085341.** Engine Namba: **2KDA438078.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/145713/2023.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**EMMANUEL ROBERT KASHINJE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC.557 DAS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya Polisi. **KAH/RB/296/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ATHUMANI MOHAMED MAVURA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba **T 628 CVR.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/154352**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ROACTIVE INDEPENDENT GROUP LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA **NISSAN UD TIPPER** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 449 DG U.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI. **KAH/TR /RB/279/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PHINA A. SHAO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **TVS** yenye usajili namba **MC 390 CSE** na CHASSIS NAMBA: MD625AF461K06084. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/OST/RB/155492/2023**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA. 1 YA 2023**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**

**CALVIN AITAEL MAIMU..........................MAREHEMU**

**NA**

**NARINDWA CALVIN AITAEL MAIMU...........MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75 na 76)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hilo katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji alietajwa hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 15 mwezi Mei mwaka 2023.
Imetolewa leo tarehe 02 mwezi wa Mei 2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**

**SHAURI NO. 11/2023**

**CHRYSPINE MACHESHA..................................MDAI**

**DHIDI YA**

1. **MARY KUSENA KUMOTA............................MDAIWA**
2. **KUMEKUCHA SACCOS LIMITED................MDAIWA**
3. **ORDER AUCTION MA...............................MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: MARY KUSENA KUMOTA**

Fahamu kwamba **CHRYSPINE MACHESHA** amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 22/05/2023 saa 2:30 asubuhi mbele ya T. Munzere Mwenyekiti wa Baraza. Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka: Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/ muhuri wa baraza hili leo tarehe 02/05/2023

T. Munzerere
MWENYEKITI
02/05/2023

---

**LAND DISPUTE COURTS (THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL)**
**GN NO.174**
**FORM NO.2B**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA TUNDURU**
**MAHALI TUNDURU**

**MAOMBI NO. 13/2023**

**OMARI SAIDI MOHAMEDI ..........................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**TUMAINI AFWILILE MWAYOLE................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA TUMAINI AFWILILE MWAYOLE**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa hukumu tarehe 25 mwezi Mei mwaka 2023 saa mbili na nusu asubuhi mbele ya mheshimiwa I.J. AYO Mwenyekiti wa baraza.

Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa. Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa baraza hili leo tarehe 28 mwezi April mwaka 2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
TUNDURU.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZEDEKIA THEODORY NGOWI** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya Gari aina ya **TOYOTA MARK II** yenye namba za usajili **T 876 CGC** (CHASSIS **NO.GX106058336)** yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **MOR/MOR/RB/153598/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKMA YA MWANZO YA (W) BOMANI-IRINGA**

**KUITWA SHAURI MDAIWA (MCA/84) (R:E 2002)**

**SHAURI LA MADAI YA TALAKA 14/2023**

**MDAI: SIJALI CLEOPHACE ZIKANKUBA**

**MDAIWA: MARLYN SAMWELI SESAN**

Shauri la madai ya talaka tajwa hapo juu limefunguliwaq katika mahakama hii tarehe 20/04/2023 na mdaiwa mtajwa hapo juu, Mdai akiomba kuachana na mdaiwa.

Hivyo basi unaamriwa wewe mdaiwa popote pale ulipo kuhudhuria hapa Mahakamani siku ya Ijumaa tarehe 11/05/20223. Saa 2:30 asubuhi bila kukosa siku hiyo kwa ajili ya kujibu madai hayo.

Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikiliza shauri hilo, ni lazima kuleta nyarata na Ushahidi wako kwa ajili ya kujitetea, Usipofika bila taarifaaaaaa shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa hukumu.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo **Tarehe 04/05/2023.**

**HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO BOMANI**
**IRINGA**
**MUHURI WA MAHAKAMA.**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa bianadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

# MAITI KWENYE KIROBA-7

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

***MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa bianadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.***




****************************************

Mgeni akajikaribisha mwenyewe kwenye kiti.

Hakuwa mwingine ila ni Inspekta Frank. Aliamua kwa dhati kumuongeza mtu ambaye alikuwa na hakina kuwa anaweza kuifanya kazi hii kwa ufanisi mkubwa.

Mtu ambaye taifa linamtegemea kwa kesi kubwa za kipelelezi ndani ya nje ya nchi. Amefanya nyingi, lakini za kukumbukwa na hasa za ndani ni zile ambazo zilisimuliwa kwenye hadithi zilizotoka kwenye gazeti la Nipashe 'Mauaji Harusini', 'Muuaji ni Nani', 'Kisanduku Cheusi', Ajenda ya Siri', na zingine nyingi ambazo alipeleleza kupata wahusika waliofanya matukio ambao walitumia nguvu kubwa na gharama kujilinda, ikiwemo hata kuajiri watu wenye uwezo mkubwa wa sanaa za mapigano.

Lakini kwa mwamba huyu walishinda na wahusika walipatikana na sasa wanatumikia kifungo. Huyu si mwingine ila ni Eddy Kamal.

"Bwana Kamal, mimi nimekuita hapa kwa kazi moja tu. Kwetu imekuwa ngumu, lakini mimi ninavyokujua na historia ya nchi hii inavyokutambua, haitokuwa ngumu kwako.

Nadhani umeshasikia miezi miwili iliyopita kumetokea mauaji ya dada mmoja hivi anaitwa Tessy. Huyu aliuawa na kukatwakatwa viungo vyake vitatumbukizwa kwenye kiroba na kutupwa maeneo ya Kinondoni Msisiri. Tumehangaika sana, ikiwa ni pamoja na kuwakamata washukiwa ambao ni waokota makopo ya plastiki pamoja na wazoa taka. Cha ajabu ni kwamba watano baada ya kuwatikisa kidogo watano wamekiri kufanya tukio hilo, lakini baadaye tukaja gundua kuwa walikiri kwa sababu ya kibano kwa sababu kila mmoja anasema aliua yeye. Wengine tumewaachia, tumewabakisha hao watano, labda tunaweza kupata mmoja kati hao."

Inspekta Frank aliongea kwa kifupi, lakini ni yalikuwa maneno yaliyojitosheleza angalau Eddy ajue ni nini chanzo cha wito ule.

Akashusha pumzi kama mtu ambaye amepewa kazi kubwa na nzito. Akatabasamu kidogo, kisha akaongea.

"Afande ina maana hakuna mtu yoyote wa kumpa isipokuwa mimi?"

"Hapana, ila mimi hizi kelele za wakubwa, pamoja na wananchi kuwa mhusika atapatikane mara moja, ndiyo zinazonifanya nione mtu pekee ambaye anaweza kuifanya kazi hii kwa muda mfupi na kwa usahihi zaidi ni wewe. Na kwa kuwa nakufahamu na ni rafiki yangu ndiyo maana nimemuomba."

"Lakini si wapo ambao wanafanya kazi hii?"

"Ndiyo, nina vijana wangu hapa, Sajenti Moses na Koplo Ben. Wanafanya vema, lakini nilitaka na wewe uingie kwenye hii kesi ili kazi iishe mapema, nakuamini mwamba, usiniangushe."

"Okay, mimi nimekubali. Nimekubali kwa sababu ya tukio lenyewe lilivyo, limeteka sana hisia za watu, lakini vile vile wewe ni rafiki yangu sana, lisipofanikiwa, au likienda kwa kusuasua, wewe ndiyo utakaolaumiwa na mimi sitaki hilo likutokee. Nataka uonekane ni mchapakazi hodari na wakuongeze hata cheo..."

Inspekta Frank aliangua kicheko na wakagongeana mikono na Eddy.

"Sasa tunafanyaje, niwaite hawa maafande wangu ili wawe chini yako mfanye hii kazi au vipi?

"Hapana afande. Mimi kama kawaida yangu, mwenyewe unanifahamu, sitaki kuchanganyika na mtu yoyote yule. Nitaifanya peke yangu."

"Na vipi Eddy, wao wasimame wakupishe, au waendelee?" "Acha waendelee. Wao waendelee na upelelezi kama kawaida tu kivyao, na mimi nitafanya kivyangu. Na sitaki hapa nikutane nao, ila waambie tu kuwa Eddy sasa yupo kazini.

Cha umuhimu hapa ni kwamba, idara yenu na yetu zinaingiliana, hivyo kama umeniomba, iandikwe barua rasmi kupelekwa kwa wakubwa wangu. Wao watatoa ruhusa na mimi kuanza kazi, ili lolote likitokea liwe rasmi kimaandishi na kwa manufaa mapana na taifa na wananchi kwa ujumla." Eddy akakumbusha.

"Nashukuru sana Eddy, ukweli sikutegemea kama ungekubali kirahisi hivyo. Hilo ondoa shaka, kabla ya kukupigia juzi nilikaa kikao na wakubwa zangu nikatoa ushauri huo wakaniambia kama atakuwa yupo tayari basi aifanye tu."

"Okay sawa, basi acha niende, nikipata ruhusa rasmi nitaianza mara moja na kuna hatua ambazo zitakuwa nakwambia, lakini kumbuka pia kuna hatua ambazo hazitakiwi kuwekwa wazi, labda mpaka mwisho." Eddy alisema na kusababisha wote wawili kuangua vicheko kwa mara nyingine tena.

**Inspekta Frank alibaki na furaha moyoni wimbo mdomoni. Alijua ameutua mzigo kwa mtu anaye ana uwezo wa kubeba mizigo mizito.**

Inspekta Frank alibaki na furaha moyoni wimbo mdomoni. Alijua ameutua mzigo kwa mtu anaye ana uwezo wa kubeba mizigo mizito.

Hakuna kesi yoyote au upelelezi wowowe uliowahi kushindwa. Alijua kabisa kuwa kesi sasa imepata mtu. Wakati wao wanaiona ni ngumu, lakini kwa Eddy Kamal, ana aina yake ya upelelezi uliochanganyikana na kipaji cha hali ya juu, baadaye inaonekana ilikuwa ni rahisi. Kifupi ni kwamba alifahamu fika kuwa upele umempata mkunaji.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# AZAM YAJIPANGA KULIPA KISASI KWA SIMBA KESHO

**Faustine Feliciane na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kumaliza machungu, benchi la ufundi la Azam FC limetangaza litapambana kusaka ushindi katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Simba itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani, Mtwara imeelezwa.

Azam FC ilifungwa bao 1-0 na Simba katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya msimu wa mwaka juzi.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa Azam, Kally Ongala, alisema wachezaji wao wana morali kubwa kuelekea katika mchezo huo na wanaamini ndoto zao za kubeba taji hilo msimu huu litatimia.

**Kally alisema kila mchezaji ameahidi kupambana kuhakikisha wanapata ushindi mapema huku wakiwaheshimu Simba ambayo bado ina joto la mashindano ya kimataifa.**

"Itakuwa ni mechi ya kulipa kisasi, hatutakubali tutolewe kirahisi na Simba, lengo letu ni kupambana kuhakikisha tunaingia hatua ya fainali," alisema Ongala.

Aliongeza wameimarisha safu yao ya ushambuliaji ili wapate matokeo mazuri na wanawataka mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi uwanjani kuwaunga mkono kwa sababu wamejipanga kuwapa furaha.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr, ameweka wazi wamejipanga kusaka ushindi baada ya kushindwa kufanya hivyo kwenye michezo miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara waliyokutana.

Beki huyo alisema moja ya malengo yao kwa sasa ni kuhakikisha wanachukua ubingwa wa kombe hilo na wanafahamu umuhimu wa mchezo huo.

"Tunajua mchezo utakuwa mgumu, lakini kama wachezaji tumeapa kujituma na kupata ushindi ili tusonge mbele, huu ni mchezo muhimu sana kwetu, tunawahidi mashabiki wetu tutapambana kuhakikisha tunasonga mbele na kucheza fainali ya FA," alisema Zimbwe Jr.

# *Geay ang'ara Mbeya Tulia Marathon*

**Mwandishi Wetu,** MBEYA

MWANARIADHA anayeshikilia rekodi ya taifa ya marathoni, Gabriel Geay, ameng'ara katika mbio umbali wa mita 1,500 za Mbeya Tulia Marathoni (MTM), zilizofanyika kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini hapa.

Mbeya Tulia Marathoni zimeanza jana na zitafikia tamati leo kwenye mbio za barabarani za kilomita 42, kilomita 10 na kilomita tano zikiongozwa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson.

Katika mbio hizo ambazo zimedhaminiwa pia na Kampuni ya Michezo ya kubashiri matokeo ya Betika, mwanariadha Faraja Lazaro alimaliza katika nafasi ya pili.

Kabla ya kuhamia kwenye marathoni, Geay alikuwa akichuana na Faraja kwenye mita 1500 mara nyingi na amewahi kuwa bingwa wa taifa kwa miaka kadhaa iliyopita.

Akizungumzia mbio hiyo hivi karibuni, Dk. Tulia alisema inalenga kukusanya fedha ili kuboresha miundo mbinu ya afya na elimu huku wakiwashukuru Betika kwa kuwadhamini wanariadha 60 msimu huu.

"Tulifanya sodo (Ligi ya soka ya mchangani), sasa tunasapoti riadha kwa kuwadhamini washiriki 60 kushiriki mbio ya Mbeya Tulia Marathoni 2023,"ilisema taarifa ya Betika.

Taarifa hiyo iliongeza wamesapoti mbio hiyo ili kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kusaidia michezo hapa nchini.




Mwanariadha, Gabriel Geay, akishangilia huku amejifunika bendera ya Twende Kibingwa baada ya kumaliza mshindi katika mbio za Mbeya Tulia Marathon (MTM 2023), zilizofanyika kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya. Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya Betika ni wadhamini wa mbio hizo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simba Queens, JKT Queens vita yakolea

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili yaliyofungwa na straika Mkenya, Jentrix Shikangwa na lingine la Asha Djaffar liliipa Simba Queens ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Alliance Girls katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi.

Ushindi huo unawapandisha tena Simba Queens hadi nafasi ya pili baada ya kufikisha pointi 39, moja tu nyuma ya vinara, JKT Queens yenye pointi 40, kila timu ikiwa imebakisha mechi mbili kabla ya kumalizika kwa msimu wa ligi.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema mpaka sasa hawajakata tamaa na wataendelea kupambana hadi mechi ya mwisho ambazo ndio zitaamua nani atakuwa bingwa.

"Niwaambie tu watu kuwa yoyote atakayekuwa bingwa msimu huu, akienda kucheza michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) pia anaweza kuwa bingwa huko, kwa sababu ametoka kwenye ligi ngumu sana," alisema kocha huyo raia wa Uganda.

Wakati JKT Queens ikiwa imebakisha mechi dhidi ya Fountain Gate Princess na Mkwawa Queens, Simba Queens wao watamaliza msimu kwa kuwakabili Baobab na Ceasiaa Queens.

## Mapinduzi FC mabingwa wa RCL 2022/2023

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mapinduzi FC ya Mwanza imetwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa wa Mikoa baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Kiluvya FC ya Dar es Salaam katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Majengo, Moshi, Kilimanjaro juzi.

Hata hivyo, timu hizo zote zimefanikiwa kupanda Ligi Daraja la Pili 'First League', kwa mujibu wa kanuni.

Wakati Mapinduzi FC ikitwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Mkoa, Nyumbu FC ya Pwani imemaliza katika nafasi ya tatu kwa kuifunga Tanesco FC ya Kilimanjaro mabao 2-1, mechi iliyochezwa awali kabla ya pambano la fainali.

Kwa matokeo hayo, Nyumbu FC itakwenda kucheza mechi ya mchujo na timu ya Daraja la Pili kwa ajili ya kusaka nafasi moja ya kupanda.

Mabingwa hao, walikabidhiwa kombe lao na Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi, Steven Mguto, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika fainali hiyo iliyoshirikisha timu nane ambazo zilipangwa kwenye makundi mawili.

## ZISIKUPITE

### NEYMAR ATAKIWA NEWCASTLE

WAMILIKI wa Newcastle United wanavutiwa na mshambuliaji wa Paris St-Germain na Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 31, wakati wanatazamia kufanya usajili wa mkubwa msimu huu wa joto. (*90min*)

### MESSI ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inafikiriwa kuwa miongoni mwa klabu zinazotaka kumsajili fowadi wa Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 35 mara mkataba wake na PSG utakapokamilika msimu huu wa joto. (*football London*)

### WOLVES WAMTAKA FATI

KLABU ya Wolves inaweza kuwapa Barcelona euro milioni 30 pamoja na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Ruben Neves mwenye miaka 26 ili wampate nyota wa Hispania, Ansu Fati (20). (*Relevo*)

### AMRABAT ANUKIA BARCA

BARCELONA imeelekeza nguvu zake katika kumsajili kiungo wa kati wa Morocco, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 26 kutoka Fiorentina, jambo ambalo linaweza kuongeza matumaini ya Arsenal kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi (24), kutoka Real Sociedad. (*AS*)

### RASHFORD, UNITED KITAELEWEKA

KLABU ya Manchester United inapiga hatua nzuri katika mazungumzo kuhusu mkataba mpya wa mshambuliaji wa England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 25, kwa matumaini ya kumuunganisha na mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane (29). (*Telegraph*)

### ARSENAL, VILLA VITANI

ARSENAL na Aston Villa ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia winga wa Barcelona, Ferran Torres, mwenye umri wa miiaka 23. (*Talksport*)

### VLAHOVIC KUTUA EPL

KLABU ya Aston Villa inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Juventus na Timu ya Taifa ya Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 23. (*Telegraph*)

### MILNER AINGIA SOKONI

KLABU ya Brighton & Hove Albion ina uhakika wa kumsaini kiungo wa kati wa zamani wa England, James Milner mwenye umri wa miaka 37 msimu huu wakati mkataba wake utakapokamilika Liverpool, ambao wameongeza juhudi zao za kumnunua kiungo wa kati wa Argentina, Alexis Mac Allister (24). (*Guardian*)

### FULHAM KUMUUZA PALHINHA

FULHAM itataka zaidi ya pauni milioni 50 msimu huu wa joto kwa kiungo wa kati wa Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 27, ambaye analengwa na Liverpool na Bayern Munich. (*Football Insider*)

### THURAM SAFARI IMEIVA

KLABU ya Newcastle United iko katika nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, Khephren Thuram, mwenye umri wa miaka 22 kutoka Nice, ambaye atakuwa tayari kwa ofa ya pauni milioni 60 msimu huu. (*Football Insider*)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KICHAPO CHA UNITED CHAMKERA TEN HAG

**Kocha huyo asema wachezaji wake walipoteza nafasi na umakini katika...**

**BRIGHTON,** England

ERIK ten Hag alionyesha "hasira" za wazi baada ya Brighton & Hove Albion kupata ushindi dakika za nyongeza na kuifanya Manchester United kuwa kwenye hatari ya kukosa kupata nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

**Kiungo wa Seagulls hao, Alexis Mac Allister, alifunga kwa penalti katika dakika ya tisa ya muda ulioongezwa baada Luke Shaw kunawa mpira eneo la hatari na VAR ikathibitisha ni penalti.**

Kipigo cha bao 1-0 kwenye Uwanja wa Amex kilidhoofisha matarajio ya United katika nafasi nne za juu, na kuwaacha pointi nne tu juu ya Liverpool walio nafasi ya tano, pamoja na mchezo mmoja mkononi.

Hag Ten alikubali upande wake ulichangia kuanguka kwao wenyewe wakati wa mechi hiyo iliyokuwa na ushindani mkubwa.

Mholanzi huyo alihisi wachezaji wake hawakuwa makini ambapo, Antony alipoteza nafasi ya dhahabu kabla ya kipa, David De Gea kuokoa mkwaju wa winga wa Albion, Kaoru Mitoma kufuatia pasi mbovu kutoka kwa Victor Lindelof.

"Kila kushindwa ni jambo linaloumiza, lakini unapopoteza katika sekunde ya mwisho, bila shaka hiyo inakera sana," alisema Ten Hag.

"Na nadhani dakika ya kwanza inajumlisha kila kitu. Tunatengeneza nafasi nzuri, hatukuwa vizuri kiafya vya kutosha, kisha kwenye safu ya ushambuliaji baada ya kuruhusu nafasi kubwa kwa zawadi kutoka kwetu.

"Na mwishowe, pia tulitoa bao na hiyo inakera kwa sababu ikiwa huwezi kushinda kwa sababu haujamaliza nafasi zako basi usipoteze."

Ushindi wa Brighton ulilipiza kisasi maumivu ya penalti waliyopata kutoka kwa wapinzani wao katika nusu fainali ya Kombe la FA siku 11 tu zilizopita na kukamilisha mechi mbili za ligi dhidi ya United.

Ushindi wa vijana wa Roberto De Zerbi uliwapandisha hadi nafasi ya sita kwenye msimamo, juu ya Tottenham na Aston Villa, na pointi nne nyuma ya Liverpool ya Jurgen Klopp walio katika nafasi ya tano.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,109,9
MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
LEEDS
1 | 1.18
X | 6.32
2 | 11.41
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# PSG YALAANI MASHABIKI WALIOMTUKANA NEYMAR



**PARIS,** Ufaransa

MABOSI wa Paris St Germain wamelaani vitendo vya mashabiki wanaodaiwa kukusanyika nje ya nyumba ya Neymar na kuimba nyimbo za kumtaka aondoke katika klabu hiyo.

Imekuwa wiki ya msukosuko kwa klabu hiyo ya Ligue 1, ambayo ilimsimamisha, Lionel Messi kwa wiki mbili baada ya safari isiyoidhinishwa ya kwenda Saudi Arabia na kuona matumaini yao ya ubingwa yakitiwa doa kwa kufungwa nyumbani na Lorient Jumapili iliyopita.

Mashabiki walirekodiwa Jumatano wakiitaka bodi hiyo kujiuzulu nje ya makao makuu ya klabu kabla ya video zaidi kuonyesha kundi la mashabiki wengine wakiwa nyumbani kwa Neymar wakimweleza aondoke.

Messi pia aliaminika kuwa mlengwa wa kukatishwa tamaa na mashabiki wakiimba wakimtaka mshindi huyo wa Kombe la Dunia aondoke, baada ya kumdhihaki nyota huyo wa Argentina katika mechi za nyumbani.

"Paris Saint-Germain inalaani vikali vitendo visivyovumilika na vya matusi vya kikundi kidogo cha watu vilivyofanyika Jumatano," taarifa ya klabu ilisema.

"Chochote tofauti za maoni, hakuna kinachohalalisha vitendo kama hivyo.

"Klabu inatoa msaada wake kamili kwa wachezaji wake, wafanyakazi wake na wale wote wanaolengwa na tabia hiyo ya aibu."



## *Napoli yasubiri miaka 33*

**NAPLES,** Italia

KLABU ya ilishinda taji lake la kwanza la Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa kipindi cha miaka 33 walipotoka sare na Udinese kwenye Uwanja wa Dacia Arena na kuibua shangwe kubwa huko Naples.

Walishinda ligi mara ya mwisho mwaka wa 1990 huku timu iliyoongozwa na Diego Maradona ikiongeza taji lao la kwanza miaka mitatu nyuma.

Victor Osimhen alifunga bao la kusawazisha dakika ya 52 baada ya Sandi Lovric kuipatia Udinese bao la kuongoza.

Napoli walishikilia hatua waliyohitaji kushinda taji lao la tatu la Serie A zikiwa zimesalia mechi tano.

"Kuona wana Napoli wakiwa na furaha inatosha kukupa hisia ya furaha wanayohisi," bosi wa Napoli Luciano Spalletti aliiambia DAZN.

"Unajisikia utulivu zaidi ukijua kuwa umewapa wakati huu wa furaha."

Napoli inamaliza miongo mitatu ya maumivu baada ya mataji mawili ya awali ya Napoli yalikuja katika siku za nguli wa Argentina Maradona (1987 na 1990) - ambaye uwanja wao sasa unaitwa umepewa jina lake.

## HABARI MICHEZO


75,029/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/05/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Aston Villa | 2.85 | 3.15 | 2.36 |
| 02. 06/05/23 | 18:00 | OGC Nice vs Stade Rennes | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 03. 06/05/23 | 19:00 | AS Roma vs Inter Milano | 2.60 | 3.05 | 2.65 |
| 04. 06/05/23 | 21:45 | US Cremonese vs Spezia Calcio | 2.20 | 3.25 | 3.05 |
| 05. 06/05/23 | 22:00 | RC Lens vs Olympique Marseille | 2.23 | 3.40 | 2.90 |
| 06. 07/05/23 | 00:00 | CA Belgrano vs Atletico Tucuman | 2.20 | 2.95 | 2.90 |
| 07. 07/05/23 | 02:30 | Charlotte FC vs New York City FC | 2.41 | 3.05 | 2.55 |
| 08. 07/05/23 | 02:30 | San Jose Earthquakes vs Los Angeles FC | 2.60 | 3.20 | 2.26 |
| 09. 07/05/23 | 02:30 | Inter Miami CF vs Atlanta United FC | 2.36 | 3.15 | 2.50 |
| 10. 07/05/23 | 13:30 | Umraniyespor vs Sivasspor | 2.75 | 3.15 | 2.16 |
| 11. 07/05/23 | 13:30 | Atalanta BC vs Juventus Turin | 2.31 | 3.25 | 2.85 |
| 12. 07/05/23 | 16:00 | FC Nantes vs Strasbourg Alsace | 2.50 | 3.30 | 2.60 |
| 13. 07/05/23 | 16:00 | AJ Auxerre vs Clermont Foot 63 | 2.25 | 3.20 | 3.00 |
| 14. 07/05/23 | 16:00 | FC Lorient vs Stade Brest 29 | 2.22 | 3.40 | 2.90 |
| 15. 07/05/23 | 17:30 | Maritimo Madeira vs Rio Ave FC | 2.43 | 3.00 | 2.90 |
| 16. 07/05/23 | 18:30 | Newcastle United vs Arsenal FC | 2.40 | 3.40 | 2.65 |
| 17. 07/05/23 | 20:00 | Vitoria SC Guimaraes vs FC Vizela | 2.31 | 3.10 | 3.00 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 06/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3831 | Karlsruher SC vs Hannover | 1.75 | 3.84 | 4.04 |
| 15:00 | 1341 | Modena vs Bari | 2.67 | 2.99 | 2.62 |
| 15:00 | 1370 | Cittadella vs Benevento | 1.85 | 3.09 | 4.40 |
| 15:00 | 1641 | Pisa vs Frosinone | 1.94 | 3.24 | 3.76 |
| 15:00 | 3686 | Genoa vs Ascoli | 1.51 | 3.75 | 6.24 |
| 16:00 | 1470 | Bordeaux vs Caen | 2.00 | 3.30 | 3.50 |
| 16:00 | 1490 | Chambishi FC vs Kansanshi Dynamos | 3.35 | 2.83 | 2.18 |
| 16:00 | 3803 | Nchanga Rangers vs Zesco United | 5.35 | 3.03 | 1.69 |
| 16:00 | 4278 | Red Arrows vs Lumwana Radiants | 1.78 | 3.02 | 4.60 |
| 16:00 | 5780 | AC Milan vs Lazio | 1.90 | 3.25 | 3.90 |
| 16:30 | 1481 | SC Freiburg vs RB Leipzig | 3.70 | 3.50 | 1.87 |
| 16:30 | 2919 | Hoffenheim vs Eintracht Frankfurt | 2.28 | 3.40 | 2.80 |
| 16:30 | 4958 | Augsburg vs Union Berlin | 3.20 | 3.15 | 2.17 |
| 16:30 | 5182 | Monchengladbach vs VfL Bochum | 1.85 | 3.70 | 3.60 |
| 16:30 | 5340 | Hertha BSC vs Stuttgart | 2.95 | 3.30 | 2.23 |
| 17:00 | 2446 | Manchester City vs Leeds | 1.18 | 6.32 | 11.41 |
| 17:00 | 2753 | Tottenham vs Crystal Palace | 1.76 | 3.75 | 3.90 |
| 17:00 | 4028 | Motherwell vs Kilmarnock | 2.15 | 3.31 | 3.15 |
| 17:00 | 4920 | Bournemouth vs Chelsea | 3.19 | 3.24 | 2.14 |
| 17:00 | 5234 | Wolverhampton vs Aston Villa | 2.84 | 3.09 | 2.41 |
| 17:15 | 4293 | Palermo vs Spal | 1.86 | 3.35 | 3.93 |
| 17:30 | 3425 | Santa Clara vs Gil Vicente | 2.76 | 3.11 | 2.49 |
| 18:00 | 3809 | Nice vs Rennes | 2.48 | 3.15 | 2.70 |
| 19:00 | 1460 | Roma vs Inter | 2.95 | 3.00 | 2.39 |
| 19:00 | 5913 | Antalyaspor vs Besiktas | 3.42 | 3.32 | 2.03 |
| 19:15 | 5887 | Brugge vs Union Saint Gilloise | 2.15 | 3.42 | 3.05 |
| 19:30 | 1652 | Werder Bremen vs Bayern Munchen | 6.65 | 5.17 | 1.34 |
| 19:30 | 4312 | Leganes vs Huesca | 2.08 | 2.91 | 3.76 |
| 19:30 | 4533 | Liverpool vs Brentford | 1.49 | 4.35 | 5.29 |
| 19:30 | 4975 | Tenerife vs Levante | 3.01 | 2.91 | 2.42 |
| 19:45 | 3477 | Sparta Rotterdam vs PSV Eindhoven | 5.39 | 4.30 | 1.49 |
| 20:00 | 1066 | Marumo Gallants FC vs Mamelodi Sundowns | 3.72 | 3.09 | 2.01 |
| 20:00 | 1586 | Niort vs Metz | 5.39 | 3.75 | 1.57 |
| 20:00 | 2525 | Boavista vs GD Estoril | 2.03 | 3.31 | 3.46 |
| 20:00 | 2944 | Nimes vs Valenciennes | 2.19 | 3.16 | 3.16 |
| 20:00 | 3066 | Amiens vs Sochaux | 2.80 | 3.15 | 2.41 |
| 20:00 | 3496 | Annecy FC vs Dijon | 3.24 | 3.04 | 2.21 |
| 20:00 | 4608 | St Etienne vs Guingamp | 1.59 | 3.85 | 4.99 |
| 20:00 | 4734 | Laval vs Bastia | 2.60 | 3.00 | 2.70 |
| 20:00 | 4984 | Reims vs Lille | 3.20 | 3.55 | 2.02 |
| 21:00 | 1816 | Cambuur vs Utrecht | 3.89 | 3.74 | 1.77 |
| 21:00 | 4204 | NEC Nijmegen vs Heerenveen | 2.11 | 3.41 | 3.11 |
| 21:30 | 3371 | SV Darmstadt vs St. Pauli | 2.07 | 3.54 | 3.18 |
| 21:30 | 5195 | St. Gallen vs BSC Young Boys | 3.37 | 3.79 | 1.91 |
| 21:45 | 1067 | Standard Liege vs KAA Gent | 3.10 | 3.41 | 2.13 |
| 21:45 | 3391 | Cremonese vs Spezia | 2.27 | 3.29 | 2.89 |
| 22:00 | 4250 | Lens vs Marseille | 2.26 | 3.36 | 2.85 |
| 22:00 | 5303 | Ajax vs AZ Alkmaar | 1.52 | 4.29 | 4.98 |
| 22:30 | 3062 | Benfica vs Sporting Braga | 1.54 | 4.10 | 5.20 |
| 23:00 | 2211 | Real Madrid vs Osasuna | 1.40 | 4.40 | 7.05 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# ZFF YAKERWA KUONDOLEWA 'KIHUNI' OFISI ZAKE AMAAN

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limetakiwa kuhamisha haraka ofisi yake iliyokuwa kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa, imefahamika.

Katibu Mkuu wa ZFF, Hussein Ahmada Vuai (pichani), alisema shirikisho hilo lilipokea taarifa hizo juzi na kutakiwa kutekeleza maelekezo hayo kutoka kwa Kamishna wa Idara ya Michezo Zanzibar hadi kufikia jana saa 4:00 asubuhi.

Hata hivyo, Vuai alisema hajakupokea barua yoyote juu ya kutakiwa kuhama na badala yake taarifa hizo ameelezwa kwa mdomo na kiongozi huyo wa serikali kwa madai wanatakiwa wapishe ukarabati.

"Kinachotusikitisha ni kupewa taarifa za ghafla hali ya kuwa sisi ni wapangaji katika jengo hili na tunalipa kodi kwa mujibu inavyotakiwa, kuhama sio tatizo, wangetupa muda kama walivyofanya kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba," alishangaa Vuai.

Katibu huyo alisema mpaka sasa bado hawajajua wataelekea wapi ili kuhifadhi vifaa vya ofisi wakati wakianza mchakato wa kukodi jengo lingine.

Aliongeza kutokana na hali hiyo, michezo ya Ligi Kuu Zanzibar iliyokuwa inachezwa kwenye uwanja huo sasa itahamishiwa katika Uwanja wa Mau.

Naye Kamishna wa Idara ya Michezo Zanzibar, Ameir Mohamed, alisema si ZFF peke yao ndio waliohamisha katika jengo hilo, ila ni wapangaji wote wametakiwa kuhama na tayari kampuni itakayosimamia ujenzi huo imeshakabidhiwa kazi.

Mbali za ZFF, ofisi nyingine zilizotakiwa kuhama ni Kamati ya Olimpiki (TOC), Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu, Chama cha Riadha na Chama cha Wanyanyua Vitu Vizito.



# *Yanga: Marumo hawachomoki*

INATOKA UK 24



Gomes.

"Bruno alikuja kwenye bechi letu kusalimia, kuna kocha wetu wa magolikipa (Milton Nienov) ni Mbrazil, na yeye ametoka huko, na baada ya hapo akapata nafasi ya kusalimia watu wote waliokuwa pale, siyo kama tuna mpango wa kumsajili au ameshasajiliwa," alifunguka.

Yanga ambao ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA, wana pointi 71 na wanahitaji pointi tatu tu ili kutetea taji hilo, lakini ndio wawakilishi pekee wa Afrika Mashariki na Kati waliobakia kwenye michuano ya CAF.

# Simba kumweka Dube 'kifungoni'

INATOKA UK 24

ya kuongeza umakini, ndiyo kitu kikubwa kitakachotupeleka kufikia malengo yetu, " alisema Robertinho.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema golikipa wao namba moja, Aishi Manula, atazikosa mechi zote zilizosalia za msimu huu kutokana na kutoimarika kwa afya yake.

Ahmed alisema Manula bado anauguza majeraha yake ya nyonga, hivyo kwa sasa langoni mwa timu yao, atasimama, Ally Salim au Beno Kakolanya.

"Wachezaji wote ni wazima na wanajiandaa na mchezo wa Jumapili dhidi ya Azam FC, isipokuwa Manula na Mohammed Quatarra, hawatakuwa sehemu ya michezo yote iliyosalia," alisema Ahmed.

Aliwataja wachezaji kama Clatous Chama, Mohammed Hussein na Shomari Kapombe, walipumzishwa katika mchezo uliopita ili kuhofia kupata kadi nyingine ambazo zingewakosesha mchezo wa kesho.

Mechi za Ligi Kuu zilizosalia kwa Simba ni dhidi ya Ruvu Shooting, Polisi Tanzania na Coastal Union.

Michezo
Nipashe Jumamosi Mei 6, 2023



Kichapo chamkera Ten Hag UK. 21



Beki wa Simba Queens, Fatma Issa 'Fetty Densa' akiruka kumiliki mpira katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (SWPL), dhidi ya Alliance Queens ya Mwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi. Simba Queens ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SIMBA SC**

## Simba kumweka Dube 'kifungoni'

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Robert Oliveira 'Robertinho' ameanza kupanga mikakati ya kuhakikisha mshambuliaji nyota wa Azam FC, Prince Dube, anashindwa kufunga bao katika mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA itakayowakutanisha kesho kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona ulioko mkoani, Mtwara.

Safu hiyo ya ulinzi itaongozwa na mabeki, Henock Inonga, Joash Onyango na mwingine ambaye ataonekana uwanjani.

Uamuzi huo unatokana na rekodi ya Dube kuifunga Simba katika kila mchezo ambao wanakutana.

Robertinho aliliambia Nipashe jana amewapa mbinu mpya mabeki wake katika siku za hivi karibuni huku akiwakumbusha kuongeza umakini kuelekea mchezo huo muhimu ambao taji lake linashikiliwa na Yanga.

"Tumendelea na maandalizi kuelekea katika mechi yetu dhidi ya Azam kwa sababu tuna matarajio makubwa ya kushinda kwenye mchezo huo wa nusu fainali, tunataka kushinda ili tusonge mbele, tunafahamu tunatakia kuongeza nguvu kwa sababu tunaenda kucheza na moja kati ya timu nzuri nchini.

"Tutaongeza umakini hasa kwenye safu ya ulinzi, tunaelewa kwa namna wapinzani walivyokuwa bora, washambuliaji wao wana kiu, wanajua nini ambacho wanakifanya na hasa ukiangalia rekodi za mechi ambazo zimepita dhidi yao, unaona kuna haja

INAENDELEA UK 23

# Yanga: Marumo hawachomoki

## ●●● Nabi asema Singida BS imewaongezea nguvu kuelekea katika...

**Na Faustine Feliciane**

HUKU wakitamba hakuna atakayewazuia kutetea ubingwa wa Ligi Kuu, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema mipango yake sasa ni kuongeza nguvu ili kuikabili vyema Marumo Gallants FC katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa Mei 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Yanga itaikaribisha Marumo Gallants kutoka Afrika Kusini katika mechi ya kwanza ya hat ua ya nusu fainali na baadaye itasafiri kwenda kukamilisha hatua hiyo ugenini.**

Akizungumza na Nipashe, Nabi, alisema anafahamu kila hatua katika mashindano hayo ya kimataifa ni ngumu, hivyo analazimika kuendelea kukijenga kikosi chake kwa ajili ya kusaka matokeo bora kwenye mechi zote mbili.

Nabi alisema waliingia kwenye dhidi ya Singida wakiwa na tahadhari ya kutotaka wachezaji wake wapate majeraha lakini wakilenga zaidi ushindi jambo ambalo wamefanikiwa kwa asilimia zote.

Kocha huyo alisema baada ya mipango yake kutimia kwa kupata pointi tatu dhidi ya Singida Big Stars, benchi la ufundi linaendeleza programu yake nyingine kwa ajili ya kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi ya kimataifa.

"Tulikuwa na wakati mgumu kama timu kutokana na majukumu yaliyopo mbele yetu, tulitaka ushindi lakini pia tulitaka wachezaji wetu wasiumie ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kukabiliana na wapinzani wetu (Marumo Gallants), tunashukuru jambo hilo limefanikiwa, sasa tunawasubiri wapinzani wetu," alisema Nabi.

Aliongeza akili yao sasa wameielekeza katika mchezo huo na wanapanga kumaliza kazi kwenye uwanja wa nyumbani kwa ajili ya kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutinga hatua ya fainali ya michuano hiyo.

"Kila Mwana-Yanga anatamani kuona tunaifikia hii rekodi ya kucheza fainali ya michuano hii, nguvu zetu tunazielekeza kwenye mchezo huu, tunatambua ugumu wake, lakini wote tunataka kuona tunamaliza kazi hapa nyumbani kwa kupata ushindi mzuri," Nabi alisema.

Aliongeza anafahamu pia wapinzani wao wataingia uwanjani kwa tahadhari wakiamini watamaliza kazi kwenye uwanja wao wa nyumbani huko Afrika Kusini.

"Mpira wa miguu una matokeo yasiyotabirika, lakini sisi tunapaswa kuutumia vizuri uwanja wa nyumbani ili twende Afrika Kusini tukijua nini tunakihitaji katika mchezo wa marudiano," aliongeza kocha huyo.

Kaulii hiyo ya Nabi, iliungwa mkono na msaidizi wake, Cedrick Kaze, ambaye alisema wanajiandaa kupata matokeo mazuri nyumbani kabla ya kuanza kuufikiria mchezo wa marudiano.

"Tunaendelea kuwaandaa wachezaji wetu, tunaamini uwezo wa kufanya vizuri tunao, ushindi wa jana (juzi) wa Ligi Kuu umetupa hamasa na kututuliza kuelekea mchezo huu wa Kombe la Shirikisho Afrika," alisema Kaze.

Mrundi huyo pia alikanusha tetesi za Yanga kumsajili kiungo, Singida Big Stars, Bruno

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >